# Nipashe

Ijumaa Januari 24, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581931

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


**MGAMBO** anaswa akiongoza magari akiwa na sare za trafiki, pingu, kisu

UKURASA 7



UKURASA 18

**SIMBACHAWENE** ashtukia mchezo mchafu maofisa utumishi kwa waajiriwa wageni



UKURASA 19

**TMA** yatoa hadhari ujio wa mvua na kitakachojiri

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**VIVUKO VIPYA VYAONGEZWA KUKABILI KILIO CHA WAKAZI WA KIGAMBONI**

SHIDA ya usafiri kwa wakazi wa Kigamboni, Dar es Salaam imetatuliwa baada ya jana serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)...

UKURASA WA 17

**ZANZIBAR KUONGEZA UZALISHAJI MPUNGA**

SERIKALI ya Zanzibar imesema mradi wa ujenzi wa mfumo wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde sita kisiwani Unguja na Pemba utaongeza

UKURASA WA 24

**YANGA: TUTAREJESHA FURAHA YETU KESHO**

ILI kupoza maumivu ya kutolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa Yanga...

**Wasira ataja msimamo CCM kuhusu hoja ya maridhiano**

UKURASA 2

# CHADEMA bado moto

**KAULI** kona zote za kina Lema, Boni Yai, Mrema, Mbowe; mali za wajumbe zashikiliwa hotelini; Mama wa Lissu aibuka; Askofu Bagonza alonga...

Endelea Ukurasa wa 2, 3 & 5




Freeman Mbowe



Godbless Lema



John Mrema



Boniface Jacob

# Hisabati bado shubiri ufaulu kidato cha nne

- WANAOANDIKA MATUSI WANAENDELEA
- KITUO CHA MTIHANI CHASHTAKIWA KORTINI
- 67 WAFUTIWA MATOKEO, 459 KURUDIA
- WAVULANA SAFARI HII WAJITUTUMUA UFAULU
- WATAHINIWA 15,185 NAO HAWAKUJITOKEZA



UKURASA 19

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed

MICHEZO SIMBA, TABORA UTD ZATUNISHIANA MISULI UK. 24 KATUNI UK. 6



Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Dodoma, Chifu Biringi Ali wa IV (kushoto), akimvalisha vazi la mgorore Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Stephen Wasira, wakati wa sherehe za kumkaribisha katika Makao Makuu ya Chama hicho jijini Dodoma jana baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CHADEMA bado kwawaka moto

**Na Halfani Chusi**

LICHA ya kupatikana kwa uongozi mpya, ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), bado kuna mnyukano wa chinichini unaendelea kwa makada wake ikiwamo waliokuwa wanawaunga mkono wagombea wa nafasi hiyo.

Jana asubuhi, kada wa chama hicho, Godbless Lema, aliyekuwa upande wa Tundu Lissu, aliyeibuka mshindi nafasi ya Mwenyekiti, akihojiwa na kituo cha redio cha Clouds, alisema mara ya kwanza alipoona misuguano imekuwa mikali aliwatuma watu wamwambie aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, ajitoe katika kinyang'anyiro hicho ili alinde heshima yake lakini hakufanikiwa.

Alisema baada ya uchaguzi imekuwa tofauti, heshima yake imepanda zaidi kutokana na kile alichokiita amefanikisha uchaguzi wa haki, huru na uwazi.

Lema alisema Mbowe hekima ilimwongoza kwamba uchaguzi usipokuwa wa wazi hata akishinda itaharibu heshima yake na taswira ya chama. Alisema taarifa ya kusimamia kura za Lissu ilikuwa ya kushitukiza huku akibainisha kwamba kampeni za uchaguzi huo zilikuwa ngumu kwake.

Alisema alitaka kukaa kimya na kutomuunga mkono yeyote lakini alishindwa kwa sababu aliona chama kinamhitaji Lissu na kwamba aliwashirikisha pia ndugu zake.

Pia alikumbusha kuwa aliwahi kuzungumza naye kuhusu kuondoka kwa waliokuwa makada, Dk. Willibrod Slaa, Zitto Kabwe na Prof. Kitila Mkumbo, hakukua na faida yoyote bali chama kilipata hasara.

Baada ya mahojiano hayo, wafuasi wa Mbowe walionesha kukerwa na kuandika mtandaoni huku wakitishia kueleza mambo mengi zaidi.

Wa kwanza kuandika ni Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema aliyeandika: "Kesho Mwenyezi Mungu akinijalia nitasema kwa kinywa kipana. "Taasisi ni muhimu sana! matusi na kejeli havijengi! kuishi ughaibuni havijengi," alisema."

Masaga Karoli, Mwenyekiti CHADEMA Mkoa Mbeya alimwomba Lissu awe mwenyekiti mpatanishi na muunganishi kama alivyokuwa Mbowe na asiwe na timu yoyote na akubali kuponya majeraha.

Mbowe katika matandoa wake wa X, aliandika: "Nimesoma neno la leo katika Kalenda ya KKKT kwenye Biblia kutoka Kitabu cha Yakobo 3 : 13 - 18. Limenirutubisha. Natamani nanyi mrutubishwe nalo.

"Je, ni nani mwenye hekima na akili miongoni mwenu? Basi, aoneshe jambo hilo kwa mwenendo wake mzuri na kwa matendo yake mema yanayofanyika kwa unyenyekevu na hekima. Lakini ikiwa mioyo yenu imejaa wivu, chuki na ubinafsi, basi, msijisifu na kusema uongo dhidi ya ukweli. Hekima ya namna hiyo haitoki juu mbinguni; hekima hiyo ni ya ulimwengu, na ya kidunia, tena ni ya kishetani.

"Maana popote palipo na wivu na ubinafsi, hapo pana fujo na kila aina ya uovu lakini hekima itokayo juu mbinguni, kwanza ni safi; inapenda amani, upole na huwajali watu; imejaa huruma na huzaa matunda ya matendo mema; haina ubaguzi wala unafiki. Uadilifu ni mazao ya mbegu ambazo wapenda amani hupanda katika amani."

Baadhi ya wafausi wake katika mtandoa huo, walitoa maoni yaliyoonesha ujumbe wake una ukakasi wakihusisha na matokeo ya uchaguzi.

Meya wa zamani wa Ubungo, Boniface Jocob, ambaye alikuwa wakala wa Mbowe katika uchaguzi huo, aliandika: "Kwangu umekuwa si tu kiongozi wangu wa chama bali ni mwalimu, mwanafalsafa, mkufunzi, mzazi, mlezi na rafiki wa kweli. Wewe ni mfano wa kuigwa.

"Nashukuru kwa kuniamini na kunipa jukumu la kuwa mwenyekiti wa kampeni zako katika uchaguzi mkuu wa chama Januari 2025,"

Aliendelea kusema anajua ameona, amesikia na ameshuhudia hadi sekunde ya mwisho alivyosimama naye na alivyojitoa kwa hali na mali kufanya jukumu lile lakini bahati haikuwa upande wao.

Aidha, alisema hakuwahi kufikiri au kudhani iko siku mwalimu wake wa siasa atampa yeye mwanafunzi wake kazi ya kusimamia kazi yake ya siasa.

"Hata hivyo, nachezwa na machale, ninavyokufahamu itakuwa kuna kitu ulitaka nijifunze kwenye majukumu yangu ya kusimamia kampeni zako.

"Funzo kubwa na la ajabu nitalikumbuka daima katika uchaguzi huu ni pale ulipoonieleza watu wako uliowapa jukumu la kufanya kampeni wasifanye jambo lolote bila idhini yako. Pia katika kila jambo tutakalofanya tusikiumize chama kwa namna yoyote," alisema Jacob.

Alisema mapenzi yake kwa CHADEMA na wanachama wake yalimfanya akubali kubeba jukumu hilo zito na kwamba alistahili msaada wake hata kama dunia nzima ingemsaliti.

"Ndiyo maana nilipoona kura zetu hazijatosha sikuhitaji ruhusa yako kusaini fomu ya matokeo kuwa Tundu Lissu ni mshindi.

"Na nilipokujulisha matokeo ya uchaguzi kuwa wajumbe 482 walihitaji uwe Mwenyekiti wao na wajumbe 513 wameamua ukapumzike. Watu wengine uliokuwa nao chumba cha VIP wakiwa wanalia wewe ulinyanyuka ukanikumbatia kisha ukachukua simu yako ili kupongeza na kukubali matokeo kupitia ukurasa wako wa X." alisema.

Taarifa za kuaminika zinaeleza baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu wamekwama kwenye hoteli mbalimbali baada ya kutolipwa fedha za kujikimu, huku wengine mizigo yao ikishikiliwa hadi walipe fedha za malazi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Wasira ataja msimamo wa CCM kuhusu maridhiano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Stephen Wasira, amesema chama kitaendeleza falsafa ya maridhiano na wako tayari kuunganisha mawazo yanayotofautiana ili kuendeleza misingi ya amani nchini.

Aidha, amesema anawajua wapinzani na hawampi shida kwa kuwa nchi inaendeshwa kwa hoja na si nguvu yeyote.

Hata hivyo, ameishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kukagua ardhi iliyoporwa kinyume cha sheria kwa wanakijiji irudi, kwa kuwa sera ya CCM watu wote wana haki ya ardhi bila kujali kipato chao.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye hafla ya kumpokea Makao Makuu ya CCM, Wasira alisema maridhiano yaliyoasisiwa na Rais Samia Suluhu Hassan yanakusudia kuendeleza kujenga nchi kuwa na umoja na amani.

"Sisi ni mfumo wa vyama vingi tukitofautiana tuongee na ukienda kuongea huwezi kupata kila kitu wewe, huko sio kuongea ni kupora haki, tunasema sisi CCM kwa kuwa tunathamini amani tupo tayari kuunganisha mawazo yanayotofautiana ili kupata mwafaka wa kuendeleza nchi kwenye misingi ya amani," alisema.

Alisema CCM inaamini katika ustahimilivu na kwamba mwenye matatizo aende wazungumze milango ipo wazi.

"Usije ukaja na mambo ya No reform (hakuna mabadiliko), No election (hakuna uchaguzi) hiyo sio ajenda ni amri, sasa sisi watu wazima tuna chama kikubwa zaidi Afrika hatuko tayari, tunasema twende kwenye uchaguzi tumeshafanya reform na wenzetu waende kwenye majimbo, urais tumewapiga bao wakienda watashindwa," alisema.

Alisema waende kupambana nafasi ya ubunge na udiwani na wakishinda waende kuzungumza na wataelewana.

"Tuwaambie ukweli tupo tayari kuzungumza na tupo tayari kuendesha uchaguzi huru na haki, wanasema serikali za mitaa kulikuwa na matatizo, tuseme ukweli zaidi ya nusu ya nafasi zilikuwa hazina wagombea wa upinzani," alisema.

Aligusia jinsi alivyokuwa akitajwa kwenye mitandao ya kijamii wakati wa mchakato wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa CCM na kuona Watanzania wakimtaja kuwa awekwe yeye ili apambane na hoja za wapinzani.

"Kushika dola na kushinda ni lazima, tuna wanachama milioni 12.5 ambao wamesajiliwa kwa mfumo wa kielektroniki na bado tunaendelea kusajili, huu ni mtaji wa ushindi kwa kuwa nyie ni askari wa mbele kukivusha chama hiki. Tunawaachа wale wajukuu wa kuchezea ndevu za babu sisi tunashika dola," alisema.

Alizungumzia sababu ya kuendelea kushika dola kuwa iliounganishwa na TANU na Afro Shiraz ikawa CCM, yeye alikuwapo na kwamba misingi ya kujengwa vyama hivyo ni maendeleo ya watu yapewe kipaumbele ili maisha yawe bora.

"Kuna chama kinatembea kinasema Nyerere alisema sisi ndio chama bora, wanamsingizia Nyerere leo niwaambie alivyosema maana nilikuwapo, aliposoma madhumuni yao alisema kweli hiki ni cha upinzani sio bora kwasababu tunasema sisi binadamu wote ni sawa wao wanasema si sawa kwamba wanyonge washindane na wenye nguvu, hawajashika dola wanagombana, tukiwapeleka Ikulu si watagawana hadi vikombe hatuwapeleki," alisema.

Alisema Mwalimu Nyerere aliwaambia wasifanye majaribio kwenye mambo ya nchi na kwamba wale wanaosema CCM imekaa sana madarakani watambue hakuna mkataba wa ukomo na CCM imewaletea maendeleo ikilinganishwa na wakati wa ukoloni.

**ARDHI**

Alisema suala la ardhi na haki ya Watanzania kuwa na ardhi ni msingi wa maisha na ni sera ya CCM na kwamba kuna sheria inasema ukitaka ardhi zaidi ya heka 25, wanakijiji wanapaswa kukutana na kuandika muhtasari na kupitia hatua zote hadi kusainiwa na Rais.

"Kuna watu huko vijijini wana ardhi kubwa hawana saini ya Rais hawa ni wavamizi, naomba niwaambie Wizara ya Ardhi ikague ardhi iliyoporwa kwenye vijiji kinyume cha sheria irudi kwa wanakijiji, tatizo la rushwa duniani ni hilo unapora halafu unahalalisha kwa rushwa," alisema.

Aliwataka wasiruhusu ardhi ikauzwa kama kanzu kuna hatari ya kusababisha Watanzania kukosa mahali pa kuishi.

Pia, viongozi wa CCM waache migogoro ndani ya chama na vikao vizungumze na kusikiliza matatizo ya wananchi ili kuyatafutia ufumbuzi.

Awali, Spika mstaafu wa Bunge, Job Ndugai, aliomba Wasira amfikishie salamu Rais Samia itakapofika Oktoba kwenye uchaguzi Mkuu, Dodoma imejipanga kuongoza kwa kura nyingi za Rais kutokana na kazi ya maendeleo aliyowafanyia wananchi.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Stesheni ya Dar es Salaam jana, akitokea mkoani Dodoma kwa usafiri wa treni ya umeme (SGR). **PICHA: IKULU**

# Shida ya vivuko wakazi Kigamboni yatatuliwa

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIDA ya usafiri kwa wakazi wa Kigamboni, Dar es Salaam imetatuliwa baada ya jana serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), ikishirikiana na sekta binafsi, kuzindua huduma ya vivuko viwili katika eneo la Magogoni-Kivukoni.

Mkataba wa ushirikiano huo umeingiwa kati ya TEMESA na Kampuni ya Azam Marine Ltd, ukigharimu Sh. bilioni 5.98 na utadumu kwa miaka minane kuwezesha usafirishaji abiria zaidi ya 50,000 kwa siku.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa vivuko hivyo, Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega alisema kuwapo vivuko hivyo vya sekta binafsi, hakutaondoa vivuko vya serikali, bali abiria atakuwa na nafasi ya kuchagua.

"Kivuko kisiwe kikwazo cha watu kufanya biashara zao, au wanaokwenda hospitalini na kutoa huduma mbalimbali wakashindwa kufanya hivyo kwa wakati eti sababu tu kivuko kipo upande mwingine," alisema.

Waziri Ulega alisema vivuko vilivyopo vinapaswa kukaguliwa kila wakati na ndiyo maana vikifikia muda wa matengenezo, vinakwenda kukarabatiwa.

"Niwahakikishie kwamba vivuko vile vitakapokuwa tayari vitarejea hapa (Mv Magogoni na Mv Kigamboni) vitafanya kazi kwa ushindani na hiyo itatufanya tusibweteke na tuwe wabunifu na itafanya tuwe wabunifu," alisema.

Alisema kivuko cha Azam Marine kitavusha abiria, kikitumia dakika tano hadi sita kutoka upande mmoja hadi upande wa pili.

Alisema kiu ya serikali ni kuhakikisha watu wanaovushwa katika eneo hilo wanafikia 70,000 kutoka 60,000 wa sasa.

Waziri Ulega alishauri uongozi wa Azam Marine Ltd kuangalia uwezekano wa kwenda kuwekeza katika huduma za vivuko katika maziwa yote nchini.

Pia aliwaomba wavuvi katika eneo la Magogoni-Kigamboni kufanya shughuli zao bila kuathiri uvushaji wananchi.

Vilevile, alizitaka mamlaka zinazofanya ukaguzi, ziwe zinakagua mara kwa mara ili kuweka mazingira safi na ulinzi dhidi ya vitu vinavyoharibu vivuko, zikiwamo nyavu za wavuvi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Suleiman Kakoso, aliitaka serikali kutoa nafasi kwa watalaam wa ndani katika matengenezo ya vivuko.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema uwekezaji huo utatatua kero ya abiria kuchelewa kwenda kwenye shughuli za kijamii.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala alisema mkataba huo wa miaka minane unahusisha pia ujenzi wa majengo ya kupokea na kupumzikia abiria na ofisi.

Alisema mkataba huo pia utahusisha usimikaji mageti na mfumo wa ukusanyaji nauli na vivuko vya kasi vitatu. Mkataba ni wa miaka minane, lakini una makubaliano ya kufanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu.

Kwa mujibu wa Kilahala, katika vivuko hivyo vya Azam Marine Ltd, abiria atatozwa Sh. 500 kwa safari moja.

Ujio wa vivuko hivyo, Kilahala alisema kutapunguza muda wa wastani wa dakika 45 ambazo abiria alikuwa anasubiri huduma. Sasa muda wa kusubiri huduma utakuwa chini ya dakika tano.

"Kwa sasa wakazi wa Kigamboni watakuwa na uhuru wa kuchagua kivuko ambacho wangependa kupanda kuvuka," alisema.

Aliongeza kuwa TEMESA inaendelea na utekelezaji ukarabati wa vivuko vya MV Kigamboni (umefikia asilimia 10) na Mv Magogoni (umefikia asilimia 55).

Matengenezo hayo kwa ujumla, Kilahala alisema yanagharimu Sh. bilioni 23.04.

Mkurugenzi Mtendaji wa Azam Marine Ltd, Aboubakar Aziz alisema kati ya vivuko hivyo viwili, kila kimoja kitabeba abiria 250 kwa wakati mmoja.

Alisema vivuko hivyo vitaanza kutoa huduma saa 11:00 alfajiri hadi saa 5:00 usiku na vinakadiriwa kwa saa vitahudumia abiria 5,000 kwa siku.

Sambamba na vivuko hivyo viwili, Aziz alisema vingine vinne vinaendelea kujengwa na kabla ya Mei mwaka huu vitaanza kutoa huduma.

Kwa mujibu wa Aziz, kila kivuko kina injini mbili na vimekidhi viwango vya usalama vya Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC).

Katika uwekezaji huo, Aziz alisema wamejenga majengo mapya ya kupokea na kusubiri abiria watakayotumiwa na vivuko hivyo.

Alisema Azam Marine Ltd kwa ujumla imetoa ajira za moja kwa moja 470 na inahudumia abiria milioni mbili kwa mwaka Tanzania Bara na Zanzibar.

# Mama wa Lissu afunguka ushindi wa mwanawe

## -Dada, majirani wasema CHADEMA itavuna...

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

FELISTER Hassan, mama mzazi wa Mwenyekiti mpya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu amesema amefurahishwa na ushindi wa mwanawe aliopata juzi, akitarajia kuona mabadiliko makubwa yakitokea ndani ya chama hicho.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari katika kijiji cha Mahambe wilayani Ikungi, mkoani Singida, mama huyo alisema ushindi huo umemfurahisha na anamwombea mwanawe majukumu mema ya kujenga chama.

"Baada ya kusikia mwanangu ameshinda, nilijisikia vizuri, nikapiga na vigelegele, nilifurahi sana, nikasema 'Mungu ni mwema'. Nilikuwa ninamwombea sana ashinde, nikasema 'mwanangu aingie na amjalie aendelee vizuri na kazi aliyoipata, aishi vizuri'," alisema.

Mama huyo pia alitaja sababu za mwanawe huyo kupewa jina la "Tundu", akibainisha kuwa ni la ukoo la kabila la Kinyaturu ambalo alipewa na baba yake.

Dada wa Lissu, Alu Lissu, alisema kuwa yeye pamoja na ndugu zake 10 tangu asubuhi ya Jumanne hadi saa 7:00 usiku wa kuamkia Jumatano, walikuwa wanafuatilia uchaguzi huo wa CHADEMA na kwamba juzi saa 12 asubuhi waliamka mapema kupata matokeo.

"Ni kama hatukulala tu, tulikesha tukiomba na kufuatilia uchaguzi huu. Tunamshukru Mungu maombi yetu yamekubalika hadi ndugu yetu ameshinda.

"Kwa furaha tuliyonayo hapa nyumbani ni lazima leo (juzi) tuchinje kuku na ikiwezekana hata ng'ombe," alisema Alu.

Dada huyo wa Lissu alisema ushindi wa kaka yake unakwenda kuleta mabadiliko ndani ya CHADEMA kutokana na Lissu kuwa jasiri, mpenda haki na anayetaka mabadiliko katika kazi anayofanya.

Majirani wa nyumbani kwa kina Lissu, Consolata Zacharia na Marcel Bilal, walisema CHADEMA sasa imepata jembe na mtu jasiri ambaye atakwenda kuinua chama hicho, wakidai kilikuwa kimeanza kupoteza mvuto kwa wananchi.

Katika uchaguzi huo, Lissu alipata kura 513 sawa na asilimia 51.5, akimwangusha Freeman Mbowe aliyekuwa anatetea kiti chake na Odero Charles alipata kura 482 na moja, mtawalia.

Mbowe amekiongoza chama hicho kwa miaka 21 tangu alipochukua kiti cha uenyekiti mwaka 2003, akiwa ni mwenyekiti wa tatu tangu kuanzishwa kwa chama hicho, akitanguliwa na Edwin Mtei na Bob Makani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

VISIT
ENTRY FREE
INTL TRADE EXHIBITION ON AGRO & POULTRY - GRAINS
EXHIBITORS FROM AROUND 17 COUNTRIES
AGRO & POULTRY 2025
Products on Display:
ANIMAL HEALTH | ANIMAL FEEDS | DAIRY PRODUCTS
FEEDS MACHINERY | FEEDS ADDIVITES
Grains Africa 2025
Products on Display:
FLOUR & PASTA ADDITIVES | BREAK ADDITIVES
FEED QUALITY CONTROL DEVICES | WHEAT & FLOUR ANALYSERS
SILOS | FRESH FRUITS PROCESSING SYSTEM
FEEDS MILLS | FLOUR MILLS | MILLILNG PLANTS
GRAINS PROCESSING SYSTEM
Date & Venue
23-25 January 2025
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania
Timing
10:00 AM TO 6:00 PM
For more info, Please Call
0758 571652 / 0656 482557

HABARI PICHANI

# BALOZI WA INDIA NCHINI, BISHWADIP DEY ATEMBELEA KAMPUNI YA THE GUARDIAN LTD



Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Jackson Paul (kulia), akimkaribisha Balozi wa India nchini, Bishwadip Dey alipofanya ziara katika ofisi za TGL, Mikocheni Viwandani, Dar es Salaam, jana.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (kulia), akimuonesha Balozi wa India Bishwadip Dey nakala ya toleo la gazeti la The Guardian, alipotembelea katika chumba cha habari cha TGL.



Balozi Bishwadip Dey akipata maelezo kuhusu uchapishaji wa magazeti ya TGL kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia). Wa (pili kushoto) ni Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paul.



Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paul (wa pili kushoto) na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (kushoto), wakipokea zawadi kutoka Balozi Bishwadip Dey. Kulia ni Mkuu wa Idara na Mambo ya Kisiasa wa Ubalozi huo, Lakshay Anand.




Balozi wa India, Bishwadip Dey (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na viongozi waandamizi wa TGL, baada ya kumaliza ziara yake. Kushoto kwake ni Naibu Meneja wa TGL, Jackson Paul. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

## HABARI KITAIFA

# Bagonza alonga ushindi wa Lissu

## -Asema Mbowe anastahili tuzo, atoa angalizo "waliolala sakafuni Mlimani City wasipuuzwe"...

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Dayosisi ya Karagwe ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Benson Bagonza amechambua ushindi wa Tundu Lissu na kushindwa kwa Freeman Mbowe kwenye uchaguzi wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Juzi Kamati ya Uchaguzi wa CHADEMA ilimtangaza Lissu kuwa mshindi baada ya kupata kura 513 za wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama sawa, akimwangusha Mbowe aliyekuwa anatetea kiti alichokikalia kwa miaka 21 na Odero Charles. Mbowe alipata kura 482 huku Odero akiambulia kura moja.

Kufuatia ushindi huo wa Lissu na timu iliyokuwa inamuunga mkono katika uchaguzi huo, akiwamo John Heche aliyemshinda Ezekia Wenje katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Tanzania Bara, Askofu Bagonza ameibuka na andishi lifuatalo:

**NINAANDIKA KUPONGEZA. SINA POLE ZA KUTOA.**

Ninawapongeza Mwenyekiti Tundu Lissu na Makamu wake, mtani wangu Heche. Hata mimi siamini kama mmeshinda lakini sina pa kukata rufani. Mwaka huu nina bahati sana. Makamu wote wa vyama vikubwa ni watani wangu: Steven Wasira na Heche. Kuna nini hapa? Ninajiteua kuwa mpatanishi siku wakigombana.

Ninampongeza Freeman Mbowe. Ameshinda kuliko alivyoshindwa. Ametufundisha sote. Kukubali matokeo hutokana na mchakato uliojaa uhuru, uwazi na haki. Tuzo ya MO Ibrahim inamhusu lakini iwe na bahasha nzito, siyo kupewa ubao tu.

Ninampongeza Mwakajoka na Mnyika kwa kusimamia vizuri uchaguzi usiku kucha. Hakuna kazi mbaya kama kusimamia uchaguzi. Mwulizeni Mzee Lubuva! Baada ya pongezi, nibwabwaje haya:

1. Mbowe siyo Mugabe kwa sababu Mugabe hakuwahi kushinda wala kushindwa uchaguzi. Daima aliamua apate kura ngapi.

2. Mbowe siyo Mugabe wala wale wooote waliowahi kukaa madarakani muda mrefu. Nilikuwapo wakati wa JKN; kama angegombea 1985, angeshinda. Nilikuwapo mwishoni mwa Mzee Rukhsa, Mkapa, Kikwete, JPM (Atake Asitake), na hata sasa nipo na Mama, Chifu Hangaya. Wote hawa wangegombea baada ya vipindi vyao kwisha, bado wangeshinda! Mbowe ameshindwa na amekubali matokeo. Yeye ni zaidi ya "Bwawa Darasa" la siasa nchini.

3. Mbowe si Mugabe. Jamani! Si rahisi kumshinda aliye kitini. Mjinga mmoja wa chama kingine kaniandikia, "Mwamba kaamua tu kumlegezea mropokaji; angeamua kubaki wangemfanya nini?"

Nami nikamjibu, "waulize waliowahi kuamua kubaki. Toka kujadiliwa na Baraza la Mawaziri hadi kutojadiliwa na Baraza la Madiwani!" Huko si kuanguka ni kuporomoka. Mbowe kathibitisha umwamba wake.

4. Tundu Lissu siyo Trump. Wanafanana ukali wa maneno si ujinga wa kisiasa. Wote walipigwa risasi, zikawaongezea kura zao. Wapinzani wa Lissu ndani ya CDM wakapuuza risasi zake na kumwongezea huruma. Lissu ni hukumu isiyo na rufani kwa watawala wanaotumia risasi badala ya hoja. Rudisheni risasi mfukoni, nendeni shule mjifunze hoja. Wamarekani walitumia risasi, sasa wanaongozwa na "kichaa mstaarabu".

5. Tundu Lissu siyo Trump. Kwa Trump mihimili inajitegemea na ina nguvu. Hapa kwetu, mihimili inamtegemea Lissu aiseemee na kuisimanga. Mmemsahau Spika Makinda? "Mwanangu Lissu, ebu tusaidie tuondoke hapo jamani". Ninatamani Tulia atulie mbele ya Makinda apate twisheni ya kufanya kazi na Lissu.

6. Tundu Lissu na Freeman wameelewana. Wapambe wao wamenuniana. Tatizo lilikuwa moja. Tundu Lissu aliwamudu na kuwaendesha wapambe; Mwamba wapambe walimmudu na kumwendesha. Wote wawili ni somo kwetu: wapambe wanaweza kukuambia wakati gani kuingia uwanjani (Lissu), lakini hawawezi kukuambia wakati gani utoke uwanjani (Mwamba).

7. Mbowe amefuta makosa yake yooote ya miaka 21 kwa kubonyesha kitufe kimoja tu: kukubali matokeo. Lissu kachukua mkopo mkuuubwa wenye riba kubwa wakati kazungukwa na vibaka. Atamudu kurejesha mkopo huu? Neno kwa Mbowe: Ukistaafu, USTAAFU. Neno kwa Lissu: Mahaba ya kutongozea na kuolea ni tofauti na mahaba ya kuishi katika ndoa.

8. Wanachadema na Watanzania: Msiyemtaka kaja. Mliyemtaka kaja. Tuna taifa la kutunza na kustawisha. Mambo yetu hayako sawa. Walio madarakani wananung'unika. Walio nje wananung'unika. Wageni wananung'unika. Wawekezaji wananung'unika. Tusiridhiane ili hali iendelee. Turidhiane kuondoa hali hii. Watawala wa zamu, msipuuze watu kulala sakafuni Mlimani City. Kuna kitu ndani yao.

9. Wako wenye shaka na Lissu. Nami nimo. Tulio na shaka tuna bahati moja: hatuhitaji kumharibia Tundu Lissu. Yeye ana uwezo mkubwa wa kujiharibia. Tumwombee.

10. Huu ni mwaka wa uchaguzi. Kwa CCM kumaliza mkutano wake na CDM kuhitimisha uchaguzi wa ndani, taifa linaweza kuwa tayari limempata rais, chama tawala na chama kikuu cha upinzani. Penye CCM waweza kuweka CDM na penye CDM waweza kuweka CCM bila kuathiri maana ya nisemacho.

HAKI inaunganisha, DHULUMA inaligawa taifa. Salaam nyingi toka barafu za milima ya Ufaransa na Ujerumani.

Ni mimi Lwakalinda Benson Kalikawe Bagonza.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi kutoka kwa **TANZANIA PETROLEUM DEVELOPMENT CORPORATION (TPDC)** ya kibali cha ujenzi wa bomba la gesi asilia lenye urefu wa 2.4km kutokea bomba la gesi la Mwenge Mbezi beach kwenye valvu iliyopo **GOIG STENDI YA MABASI,** Barabara ya Bagamoyo kuelekea **BQ CONTRACTOR CNG STATION**, Barabara ya Goba, Manispaa ya Kinondoni. Bomba hili litatumika kusambaza gesi asilia kwenye Kituo cha kujazia Gesi Asilia Cha BQ Contractor.

Hivyo, mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MTWARA, LINDI NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MADABA, NAMTUMBO NA TUNDURU.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumanne tarehe 28 Januari hadi siku Jumatatu tarehe 03 Februari, 2025
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa leo tarehe 20 Januari, 2024 na:**

**Christina P. Ballali**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dhamira, uwajibikaji vikiwapo, magonjwa mlipuko yataepukika

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi aliwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni ikiwa ni jitihada zake za kujaza ombwe la nafasi katika utendaji au mabadiliko ya kawaida kuimarisha utendaji ambayo amekuwa akiyafanya mara kwa mara.

Katika uapisho huo, waliohusika ni majaji wa Mahakama ya Rufani ambao walipandishwa kutoka kuwa majaji wa Mahakama Kuu. Mwingine aliyeapishwa ni Dk. Grace Magembe ambaye hivi karibuni aliteuliwa kushika nafasi hiyo kuchukua nafasi ya Prof. Tumaini Nagu ambaye uteuzi wake umetenguliwa. Kabla ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo, Dk. Magembe alikuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Pamoja na kuwaagiza majaji kuwajibika na kuhakikisha haki inatendeka, kubwa zaidi aliloagiza ni kwa Dk. Magembe kwamba akasimamie udhibiti wa magonjwa ya mlipuko ambayo yana athari kubwa kwa nchi kiuchumi na kijamii.

Hivi karibuni, kwa mfano, kulikuwa na taarifa ya kuibuka kwa ugonjwa wa Malburg katika mkoa wa Kagera ambao ungesababisha watu kuzuiwa kusafiri hivyo kuwapo kwa athari kubwa. Ugonjwa huo uliwahi kuripotiwa mkoani humo na kusababisha vifo vya watu kadhaa.

Licha ya ugonjwa huo, mwaka 2020 uliibuka ugonjwa wa UVIKO - 19 ambao uliikumba dunia nzima na kusababisha vifo vya mamilioni ya watu, uchumi wa mataifa mbalimbali kuporomoka na watu kukosa kazi kutokana na uzalishaji kuwa mdogo na taasisi na mashirika makubwa kufungwa. Tanzania ilikuwa moja ya nchi zilizoathirika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa watalii kutoka mataifa mbalimbali walishindwa kusafiri na kutembelea vivutio na mbuga za wanyama.

Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana Rais Samia amemwagiza Dk. Magembe kusimamia ipasavyo magonjwa ya mlipuko ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza pindi magonjwa hayo yanapoibuka.

Licha ya magonjwa hayo makubwa ya mlipuko ikiwamo Ebola ambayo inaitesa nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), nchini Tanzania kila mwaka kumekuwa kukiripotiwa kuibuka kwa maradhi mengine ya mlipuko kama vile kipindupindu, kuhara na kuhara damu. Magonjwa hayo tariban kila mwaka yamekuwa yakiibuka maeneo mbalimbali ya nchi na sababu kubwa ni uchafu.

Ni dhahiri kwamba Rais Samia ameonesha kukerwa na kuwapo taarifa za mara kwa mara za magonjwa hayo, ndiyo maana ametoa agizo hilo kwa msisitizo mkubwa kwa sababu yana athari kubwa kwa uchumi wa nchi.

Ni kweli kwamba Rais Samia amemwagiza Dk. Magembe kusimamia suala hilo akiwa ndiye mganga mkuu kiongozi wa serikali lakini maana yake ni kwamba waganga wote wakuu wa mikoa na wilaya na wale wafawidhi wa hospitali na vituo vya afya wanahusika na jambo hilo.

Kwa maana hiyo, wote hao pamoja na viongozi waliopewa dhamana katika ngazi mbalimbali za serikali, wanatakiwa kuwajibika katika vita dhidi ya magonjwa hayo. Kushindwa kuwajibika kwao wanaweza kuchukuliwa hatua kali ikiwamo kuondolewa kwenye nafasi zao za kiutendaji.

Katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya kwa mfano, taarifa za magonjwa ya mlipuko ya kipindupindu, kuhara na kuhara damu yamekuwa yakiripotiwa takriban kila mwaka. Jambo la kujiuliza ni je, wahusika wameshindwa kusimamia ipasavyo suala la usafi mpaka maeneo hayo kuwa makao makuu ya kipindupindu?

Kuwapo kwa magonjwa hayo kila mwaka ni dhahiri kuna uzembe miongoni mwa watendaji kwa sababu wameshindwa kusimamia usafi wa mazingira na kuchukua hatua dhidi ya wananchi wanaotiririsha maji machafu nyakati za mvua. Kila mtu akiwajibika na kuwapo kwa dhamira ya dhati magonjwa hayo yatakuwa historia nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Wasichana, wanawake hawa wasaidiwe na wataalamu, kabla hawajapotea

Na Joyce Lameck

**BAADHI** ya watu wanafikiri kwamba utoaji mimba daima ni makosa. Pia, kuna wengine wanaodhani kwamba kutoa mimba ni sawa, ilhali maisha ya mama yanakuwa hatarini.

Pia kuna wengine wanaofikiri kwamba, kuna hali mbalimbali, ambazo kutoa mimba kunakubalika kimaadili.

Niseme kuwa siku zote, utoaji mimba usio salama, hauishii kuathiri afya pekee, hata kiakili. Kwa ujumla, inaishia kusababisha madhara kwa mama aliyetoa mimba, pasipo kuzingatia picha pana ya usalama wake, ikiwamo njia zisizo salama kwa kuogopa sheria, pamoja na adhabu iliyopo nchini.

Mtaalamu wa saikolojia kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, ambaye ni mtaalamu wa kutibu magonjwa ya akili, Dk. Faithness Kiondo, ana orodha ya madhara ambayo mama anayapata kiakili, pale anapotumia njia zisizo salama kutoa mimba.

Anaeleza kwamba, wanawake wengi hupatwa changamoto ya maradhi sonona, yanayotokana na msongo wa mawazo, pia upweke kifikra bila kupata suluhu ya kile anachokifikiri kila wakati.

Vilevile anasema, kuna wakati mama aliyetoa mimba kwa njia ambazo si salama, anaweza kupata hali ya kiwewe ambalo ni tatizo la kiakili lililosababishwa na wasiwasi, mhemko kama zao la tukio hilo.

Dk. Faithness anafafanua kuwa mwanamke, msichana anakuwa ni wa kuona aibu na kujiona ana hatia kila wakati, pindi anapotafakari kuhusu tukio la utoaji mimba usio salama kwani njia alizotumia hazikuwa salama na mafichoni.

Mbali na changamoto hizo, mwanasaikolojia huyo anasema kuwa, mama huyo anaishia kutumia kilevi, akiamini itamsaidia kuwa sawa kiakili, lakini kumbe inamuongezea matatizo si kiafya pekee, bali hata kiakili.

Mtaalamu huyo anaeleza kuwa mama aliyekutana na changamoto hiyo, anaweza kuchukua hatua mbaya zaidi ya kujaribu au kutaka kujiua, kutokana na msongo wa mawazo yaliyosababishwa na utoaji mimba usio salama.

Vilevile waathirika wa utoaji mimba usio salama wanakabiliwa na matatizo ya muda mrefu kama utasa na maumivu ya tumbo, hata kuharibika kwa kizazi na kubwa zaidi ni kupoteza maisha kwa mama na mtoto aliyekuwa tumboni.

Madhara hayo hutokea pale zinapotumika njia zisizo salama kutoa mimba, kwani mara nyingi hata mtoa huduma si yule mwenye elimu sahihi na kutokuwa na weledi au ufanisi wa kazi yake, hivyo hufanya bila kujali madhara ya kiakili kwa mama.

Hata hivyo, mtazamo hasi wa jamii kwa kinamama wanatoa mimba, ndio unaosababisha kuchukua uamuzi inayowapeleka kutumia njia zisizokuwa salama katika kutoa mimba na kusababisha madhara kiafya na hata kiakili.

Hata hivyo, kutokuwapo kwa elimu na uhamasishaji wa kutosha wa afya ya uzazi makundi mbalimbali na hasa vijana na wanaume kumesababisha kuongezeka kwa magonjwa ya ngono, pamoja na matatizo ya mimba zisizotarajiwa, hasa maeneo ya vijijini.

Pia, mila potofu zimechangia katika kuzorotesha afya ya uzazi katika baadhi ya maeneo nchini, hasa kwa yale ambayo bado hayajafikiwa na elimu, huduma kuhusu uzazi salama kwa mama na mtoto.

Wanawake wanaohitaji kutoa mimba wako kinyume na maadili ya kitamaduni ambayo yanajumuisha wazo kwamba ngono inatumika tu, kwa uzazi na kwamba wanapaswa kubaki safi kingono mpaka pale watakapo hitaji uzazi.

Serikali nayo kupitia Wizara ya Afya katika mapambano dhidi ya changamoto ya utoaji mimba usio salama, ikiwamo kutoa elimu juu ya afya ya uzazi kwa watoto wa kike ambao wapo chini ya umri wa kuzaa

Vilevile wizara kupitia vitengo vyake, imeendelea kutoa elimu kwa klabu za vijana na vijana balehe kutojihusisha na ngono zembe, ili kuepuka kupata mimba zisizotarajiwa ambazo hupelekea kuongezeka vitendo vya utoaji mimba usio salama.

Pia, inaendelea kusimamia utoaji wa huduma za uzazi wa mpango katika vituo vya huduma bila malipo, ili kuwawezesha wanawake na wanaume kuzuia mimba zisizotarajiwa.

Hata hivyo wajawazito kuhudhuria katika kliniki za uzazi wa mpango itawasaidia, waweze kupatiwa elimu ya afya ya uzazi ikiwamo jinsi ya kuepukana na mimba zisizotarajiwa, hata kuondokana na uavyaji wa mimba usio salama.

HABARI KITAIFA

# Mgambo akamatwa kwa tuhuma kujifanya polisi

## -Adaiwa kukutwa akiongoza malori kwenye foleni

**Na Mose Ng'wat,** SONGWE

BANGROS Sikaluzwe (37), mkazi wa Ilolo, wilayani Mbozi, amekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kwa tuhuma za kujifanya askari wa Jeshi la Polisi nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Akama Shaaba, mtuhumiwa huyo alikamatwa Januari 22 mwaka huu saa 7:45 usiku katika msako uliofanyika Mtaa wa Majengo, mjini Tunduma, katika wilaya ya Momba.

Kaimu Kamanda Akama alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa anafanya kazi za usalama barabarani katika barabara ya Tunduma-Sumbawanga kwa kuyapanga malori yanayovuka mpaka wa Tunduma kwenda Zambia na nchi nyingine za kusini mwa Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Kaimu Kamanda Akama, mtuhumiwa huyo alikutwa akiwa amevaa sare za polisi.

Pia anadaiwa kukutwa na vifaa vingine vya jeshi hilo, zikiwamo pingu alizokuwa amezining'iniza kiunoni, kisu cha kukunja na tochi aliyokuwa ameshika mkononi.

Kaimu Kamanda Akama alisema kuwa uchunguzi wa haraka ulibaini kuwa Sikaluzwe siyo askari polisi, bali ni mgambo aliyekuwa anajifanya askari kwa malengo ambayo hayajathibitishwa.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe limewaonya wananchi, waache tabia ya kuvaa sare za polisi au kujifanya askari, kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wahusika," Kaimu Kamanda Akama anaonya katika taarifa yake hiyo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# RC awataka wananchi kuchukua tahadhari maambukizi ya Marburg

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Alfred Mtambi (pichani) amewakumbusha wananchi wa mkoa huo kuchukua tahadhari kujilinda dhidi ya tishio la maambukizi ya ugonjwa wa Marburg.

Alisema kuwa ingawa hadi sasa ni mtu mmoja amegundulika kuwa na ugonjwa huo mkoani Kagera, kuna haja ya kuchukua tahadhari ili kuepukana na ugonjwa huo.

Kanali Mtambi alisema hayo wakati wa kikao cha utambulisho wa kazi na majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) mjini Musoma juzi.

"Ingawa kwa sasa ni mtu mmoja amegundulika katika mkoa wa Kagera, mgonjwa huyo anaweza kuwa ameshawaambukiza watu wengine kabla yeye hajagundulika," alisema Kanali Mtambi.

Alisema wananchi wanatakiwa kusikiliza na kufuata maelekezo ya wataalam wa afya kuhusu namna ya kukabiliana na tishio la ugonjwa huo, ikiwamo kuacha baadhi ya tabia zilizozoeleka ndani ya jamii na kurudi katika utaratibu wa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni kila wakati.

"Wataalam wa afya, wakuu wa wilaya na viongozi wa halmashauri endeleeni kutoa elimu kwa wananchi na kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na tishio la kuenea kwa ugonjwa huo," alisema.

Mwakilishi wa Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Afya, Lishe, Ustawi wa Jamii, Erick Muhigi alisema mkoa huo unaendelea na utoaji elimu kwa wananchi kuhusiana na ugonjwa wa Marburg baada ya kugundulika mgonjwa katika mkoa wa Kagera.

Muhigi alitaja dalili za ugonjwa huo ni pamoja na mwathirika kupata homa kali, kuhara au kuhara damu, kutapika na wakati mwingine kutapika damu na kutokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili.

"Ugonjwa huo unaenea kwa njia mbalimbali, ikiwamo kugusa jasho, mkojo, damu, kinyesi, matapishi, nguo, matandiko, kugusana na mtu aliyeathirika au wanyama walioathirika na ugonjwa huo," alisema.

Muhigi alisema ni muhimu wananchi kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono yao kwa maji tiririka kwa sabuni, kuepuka kugusa au kuosha maiti ya mtu aliyefariki dunia kwa ugonjwa huo na kuepuka kula mizoga ya wanyama.



"Ugonjwa huo unasambaa kwa haraka katika jamii na mtu aliyeathirika anaanza kuonesha dalili baada ya siku mbili hadi 21 na anaweza kuwaambukiza wengine hata kama hana dalili," Muhigi alitoa hadhari.

Mwakilishi huyo wa Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Afya, Lishe, Ustawi wa Jamii, alisema katika mazingira ya aina hiyo ni rahisi kusambaa kwa maambukizi katika jamii.

Aliongeza kuwa mkoa huo umeimarisha udhibiti wa wagonjwa katika Mpaka wa Sirari na vivuko vya wananchi kutoka nchi jirani, udhibiti wa Uwanja wa Ndege wa Musoma na viwanja vingine vya ndege vilivyoko katika mkoa huo.


airtel
A REASON TO **IMAGINE**

MUONGOZO WA GHARAMA ZA AIRTEL KUANZIA JANUARI - MACHI 2025

| LIPIA KADRI UNAVYOTUMIA: KODI IMEJUMUISHWA | | Bei (TSh) |
|---|---|---|
| MITANDAO YOTE | TSH/ sek | 0.50 |
| NDANI YA MTANDAO | TSH/ sek | 0.50 |
| INTANETI | TSH/ Mb | 9.35 |
| SMS ZA NDANI YA NCHI | TSH/ Sms | 8.00 |
| SMS ZA NJE YA NCHI | TSH/ Sms | 215.00 |

MITANDAO YOTE

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 30 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 150 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 150 | 50 |
| Siku 7 | 2,500 | 300 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 400 | 100 |
| Siku 30 | 10,000 | 1,200 | 100 |

BANDO ZA SMS

| Muda | Bei(TSh) | SMS |
|---|---|---|
| Saa 24 | 200 | 200 |
| Siku 7 | 500 | 1,000 |
| Siku 15 | 1,000 | 5,000 |
| Siku 30 | 1,500 | 10,000 |

MITANDAO YOTE

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti (MB) |
|---|---|---|---|---|
| BILA KIKOMO | 1,000 | 60 | 50 | |
| BILA KIKOMO | 2,000 | 20 | | 900 |

BANDO ZA INTANETI

| Muda | Bei (TSh) | (MB) |
|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 246 |
| Saa 24 | 1,000 | 492 |
| Siku 3 | 2,000 | 985 |
| Siku 7 | 2,000 | 950 |
| Siku 7 | 2,100 | 1,024 |
| Siku 7 | 3,000 | 1,480 |
| Siku 7 | 5,000 | 2,460 |
| Siku 30 | 10,000 | 4,920 |
| Siku 30 | 20,000 | 9,850 |
| Siku 30 | 30,000 | 14,780 |
| Siku 60 | 50,000 | 24,600 |
| Siku 60 | 100,000 | 49,200 |

COMBO (DAKIKA + MB)

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote(Dak) | SMS | Intaneti(MB) |
|---|---|---|---|---|
| Masaa 24 | 1,000 | 40 | 10 | 350 |
| Siku 7 | 2,000 | 55 | 10 | 800 |
| Siku 30 | 10,000 | 400 | 10 | 3,600 |
| Siku 30 | 20,000 | 500 | 10 | 8,192 |

BILA KIKOMO

MUONGOZO WA GHARAMA ZA KIMATAIFA (KODI HAIJAJUMUISHWA)

| Nchi | BAND | Bei(TSh/Sek) |
|---|---|---|
| China, Canada, India, USA | Band 1 | 480.00 |
| Malaysia, Japan, Lebanon, Nigeria,Pakistan, Yemen, United Arab Emirates | Band 3 | 600.00 |
| REST OF AFRICA, Denmark, Ireland, Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Oman, Italy, Ghana | Band 5 | 840.00 |
| Angola, Benin, Denmark, Djibout, Ethiopia, Finland, Haiti, Mali, Malawi, Zambia,Dem.Rep.of Congo, Sudan, Zimbabwe | Band 6 | 1,500.00 |
| France, Rest of World, South Africa | Band 7 | 799.80 |
| Albania, Belarus, Belgium, Bulgaria, Cameroon, Chad, Central African Republic, Comoros, Cook Islands, Congo, Sao Tome & Principe, Cuba, East Timor, Gabon, Gambia, Germany, Guinea, Guinea Bissau, Kiribati, Latvia, Somalia, Lithuania, Madagascar,Micronesia, Maldives, Moldova, Montenegro, Martinique, Nauru, Papua New Guinea, Reunion Island, Solomon Islands, San Marino, Seychelles, Sierra Leone, Senegal, Samoa, Switzerland, Tuvalu, Tonga, Uzbekistan, United Kingdom, Vanuatu, Wallis & Fatuna | Band 8 | 2,820.00 |
| Uganda | Band 10 | 178.80 |
| Kenya, Rwanda, South Sudan | Band 11 | 178.80 |
| Satellite, Inmarsat, Premium Diego Garcia, Ascension Island, St.Helena, GreenLand Falkland Islands, Tokelau, Dem. Rep. Of Congo, Special numbers, Chile, Australia Territories, Niue Island, Upt, Norfolk Island, Chile | Band 12 | 14,000.00 |

| BANDO ZA KIMATAIFA | MUDA | BEI YA BANDO (TSH) | DAKIKA |
|---|---|---|---|
| INDIA | Saa 24 | 5,000 | 60 |
| CHINA | Saa 24 | 5,000 | 20 |
| USA CANADA | Saa 24 | 1,000 | 10 |
| AFRIKA KUSINI | Saa 24 | 3,000 | 4 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Saa 24 | 2,500 | 5 |
| ULAYA | Saa 24 | 5,000 | 4 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Saa 24 | 2,500 | 3 |
| INDIA | Siku 7 | 10,000 | 150 |
| CHINA | Siku 7 | 15,000 | 60 |
| USA CANADA | Siku 7 | 5,000 | 50 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 7 | 6,000 | 7 |
| MALAWI, DRC | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| ZAMBIA | Siku 7 | 10,000 | 7 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 7 | 5,000 | 10 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 7 | 5,000 | 6 |
| INDIA | Siku 30 | 15,000 | 250 |
| CHINA | Siku 30 | 25,000 | 100 |
| USA CANADA | Siku 30 | 15,000 | 150 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 30 | 15,000 | 20 |
| MALAWI, DRC | Siku 30 | 20,000 | 15 |
| ZAMBIA | Siku 30 | 20,000 | 15 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 30 | 15,000 | 30 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 30 | 20,000 | 24 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 30 | 15,000 | 18 |

SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu | MB |
|---|---|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 5 | 5 | 75 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 25,000 | 15 | 10 | 250 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 40,000 | 25 | 20 | 500 |
| Eneo -2 | Siku 3 | 25,000 | 12 | | 250 |
| Eneo -2 | Siku 7 | 50,000 | 15 | | 200 |

SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Saa 24 | 5,000 | 500 |
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 1,299 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 15,000 | 2,048 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 30,000 | 5,120 |

SAFARI ROAMING BANDO - KUPIGA NA KUPOKEA SIMU

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu |
|---|---|---|---|---|
| Eneo -2 | Siku 7 | 10,000 | 10 | |

SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -3 | Siku 3 | 40,000 | 1024 |
| Eneo -3 | Siku 7 | 75,000 | 2048 |
| Eneo -3 | Siku 14 | 200,000 | 5120 |

SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo - 4 | Siku 3 | 35,000 | 200 |
| Eneo - 4 | Siku 7 | 90,000 | 512 |
| Eneo - 4 | Siku 14 | 175,000 | 1024 |

| | |
|---|---|
| **Eneo 1** | Kongo B(Airtel), DRC(Airtel), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel),Kenya(Airtel), Madagasca(Airtel), Malawi(Airtel), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Seychelles(Airtel), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel), India(Airtel) & Mauritius(Emtel) |
| **Eneo 2** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), KongoB(Airtel), KongoDRC(Airtel), Egypt(Orange), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel), Kenya(Airtel), Madagascar(Airtel), Malawi(Airtel), Mauritius(Emtel), Mozambique(Vodafone), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Afrika Kusini (MTN, Vodafone), Swaziland(MTN), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & **CANADA:** (Bell, Telus) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** China(China Mobile), Bangladesh(Airtel), India(Airtel), Israel(Pelephone, Cellcom), Oman(OmanTel), Pakistan(Telenor, Vimplecom), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), SriLanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE (dU, Etisalat) |
| | **ULAYA:** Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(T-Mobile), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **OCEANIA**: New Zealand(Vodafone) |
| **Eneo 3** | **AFRIKA:** Botswana(MTN), Cameroun(Orange), Egypt(Orange), Ghana(Airtel, TIGO), Ivory Coast(Moov), Mali(Orange), Mozambique(Vodacom), Mauritius(Emtel), Senegal (Orange), Swaziland(MTN), South Africa(MTN, Vodacom) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & **CANADA:** (Bell, Telus) |
| | **ULAYA:** Belgium(Base, Orange), Switzerland(Swisscom), Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(Cosmote), Ireland(Vodafone), Italy(Vodafone,Tim), Luxembourg(P&T), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Poland(T-Mobile), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** India(Airtel), Indonesia(Telkomsel), Israel(Orange, Jordan(Orange), Malaysia(Digi), Pelephone, Cellcom),Pakistan(Mobilink, Telenor), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), Sri Lanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE(Etisalat) |
| | **CHINA:** China Mobile |
| **Eneo 4** | **AFRIKA: Afrika Kusini**(Cell C) |
| | **MAREKANI:** AT&T |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** Oman (OmanTel), UAE (dU), Turkey (Turkcel) |

*Vigezo na masharti kuzingatiwa. Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu: https://www.airtel.co.tz



Mwenyekiti Mpya wa Chadema Taifa, Tundu Lissu na Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Freeman Mbowe, wakionyesha alama ya vidole viwili wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yaandika historia mpya ya demokrasia



**Na Khaled Gwiji**
**Simu: +1 437 431 6747**
**Barua pepe:**
**khaleed_ihaab@yahoo.com**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeandika historia ya kipekee na adhimu katika siasa za Tanzania, kwa kuonesha kivitendo dhana halisi ya demokrasia ya vyama vingi.

Katika mazingira ambayo mara nyingi vyama vya siasa hukumbwa na changamoto za viongozi kung'ang'ania madaraka, kuzuia ushindani wa hoja, au kuwatenga wanaoleta mitazamo tofauti, CHADEMA kimejitokeza kama alama ya matumaini kwa mustakabali wa siasa safi na zenye heshima kwa misingi ya kidemokrasia.

Kwa kuruhusu uchaguzi wa wazi, huru, na wa haki kwa viongozi wake waandamizi, CHADEMA kimeonesha kwamba ushindani wa hoja haupaswi kuwa chanzo cha migawanyiko, bali chachu ya maendeleo na mshikamano wa kitaasisi. Tukio hili linatoa funzo kubwa kwa vyama vingine nchini na barani Afrika, ambapo mara nyingi tofauti za kimtazamo zimekuwa zikigeuzwa kuwa sababu ya mifarakano badala ya maendeleo ya kijamii na kisiasa.

Katika uchaguzi wa hivi karibuni ndani ya CHADEMA, viongozi wenye ushawishi mkubwa kama Freeman Mbowe na Tundu Lissu, walishindana kwa hoja mbele ya wanachama, wakiweka mbele maslahi ya chama kuliko ya binafsi. Badala ya kugeuza ushindani wao kuwa chanzo cha chuki au migawanyiko, walionesha ukomavu wa kisiasa wa hali ya juu kwa kukubali matokeo, huku wakihimiza mshikamano wa chama baada ya uchaguzi.

**UPEKEE WA DEMOKRASIA YA CHADEMA**

Katika historia ya siasa za dunia, vyama vinavyokumbatia demokrasia ya kweli ndani ya mfumo wao wa uongozi vina nafasi kubwa ya kuaminika mbele ya umma. CHADEMA imeonesha vipengele vya kipekee vya demokrasia ambavyo ni somo kwa vyama vingine:

**1. Uwazi na Uwajibikaji:**
Kwa kuruhusu uchaguzi wa wazi uliohusisha wanachama wa ngazi mbalimbali, CHADEMA imejenga msingi imara wa kuimarisha imani ya umma katika siasa safi. Hatua hii inalinganishwa na mifano ya vyama kama Labour Party ya Uingereza au Democratic Party ya Marekani, ambavyo hufanya chaguzi za wazi kwa wagombea wake, huku vikihakikisha uwazi katika mchakato mzima wa uchaguzi.

**2. Ushindani wa Hoja Badala ya Migawanyiko:**
Badala ya kuona ushindani wa mawazo kama chanzo cha migogoro, CHADEMA imeonesha kwamba tofauti za kimtazamo zinaweza kuwa nguvu ya kuimarisha taasisi. Mfano wa aina hii unalingana na historia ya vyama kama African National Congress (ANC) ya Afrika Kusini, ambapo viongozi kama Nelson Mandela na Thabo Mbeki waliendesha mijadala ya kina ndani ya chama chao huku wakiheshimu misingi ya demokrasia.

**3. Hekima ya Kukubali Matokeo:**
Kukubali matokeo ni kitendo kinachothibitisha ukomavu wa kisiasa. Katika historia ya dunia, wanasiasa kama Al Gore wa Marekani, aliyekubali matokeo ya uchaguzi wa urais wa mwaka 2000 licha ya kutokubaliana na uamuzi wa Mahakama Kuu, ni mfano wa hekima ya kukubali matokeo kwa maslahi ya wengi. CHADEMA, kwa uongozi wake wa sasa, imeonesha ukomavu kama huo kupitia uchaguzi huu wa ndani.

**4. Kuimarisha Umoja wa Chama:**
Pamoja na ushindani mkali, viongozi wa CHADEMA walionesha mshikamano wa hali ya juu baada ya uchaguzi. Hili linafanana na mfano wa vyama kama Conservative Party ya Uingereza, ambapo wagombea mara nyingi hujipanga pamoja baada ya uchaguzi wa ndani kwa ajili ya kulinda maslahi ya chama na taifa.

**SOMO KWA TAIFA NA VYAMA VINGINE**

Mchakato wa CHADEMA unatoa funzo kubwa kwa vyama vingine vya siasa nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla. Demokrasia ya kweli haihitaji mshikamano wa mawazo, bali mshikamano wa maadili, uvumilivu wa fikra, kuheshimiana na dhamira ya dhati ya kuhudumia umma.

Katika mazingira ambako siasa mara nyingi zinatumiwa kwa maslahi ya kibinafsi, CHADEMA imejitokeza kama kielelezo cha siasa safi na kwamba utofauti wa mambo kati yetu si kasoro wala uadui, wala udhaifu. Kutokukubali kuwa tuko tofauti ndio kasoro na udhaifu wenyewe.

Mkono hutusaidia katika kazi zetu; lakini vidole vya mkono huo huo unaotusaidia havilingani; hata hivyo, vyote hufanya kazi kwa pamoja.

Kasoro ya ufupi na/au urefu wa kidole hauondoi umuhimu wa kuwa sehemu ya mkono.

Tusitafute usawa wa fikra au mitazamo–bali tukubaliane kwamba sote tupo tofauti kwa faida ya wote. Muhimu zaidi, tukubali kutofautiana katika fikra na mitazamo; lakini tubaki kuwa wamoja. Wanaozaliwa pacha wakafanana sura, rangi, jinsia na tukashindwa hata kuwabagua wanakuwa na tofauti zao–sembuse sisi tuliozaliwa matumbo mbalimbali, sura mbalimbali, malezi na makuzi lazima tutakuwa na tofauti. Hivyo basi, msingi wa kutufanya tuwe pamoja licha ya tofauti hizo ni uvumilivu na kuheshimiana na kikawaida mawili hayo hayaji bila ya maarifa.

Katika historia ya siasa za vyama vingi nchini Tanzania, tukio hili linatoa matumaini mapya. Ushindani wa hoja badala ya migawanyiko ni msingi wa maendeleo ya taifa lolote. CHADEMA imeonesha kwamba siasa za heshima na za kiadilifu zinaweza kufanikisha umoja na maendeleo.

**PONGEZI VIONGOZI, WANACHAMA CHADEMA**

Kwa dhati kabisa, tunapaswa kuwapongeza viongozi wa CHADEMA, hususan Freeman Mbowe na Tundu Lissu, kwa kuonesha mfano wa ukomavu wa kisiasa. Timu zao za kampeni pia zinastahili sifa kwa kujenga mazingira ya ushindani wa hoja badala ya migawanyiko. Wanachama wa CHADEMA wameonesha kuwa wapo tayari kuheshimu misingi ya demokrasia, na chama chao kimejitokeza kuwa taasisi yenye maono makubwa kwa taifa.

Kwa muktadha huu, CHADEMA imeandika historia itakayosomwa na kujifunza kwa karne nyingi zijazo. Hekima yao inapaswa kuwa msingi wa kujenga taifa lenye mshikamano, haki, na maendeleo endelevu. Tanzania inaweza kujifunza kutoka kwa CHADEMA kwamba demokrasia ni chombo cha kujenga, SI kugawanya.



# Ushawishi kisiasa watibua Wananchi Milima ya Pare

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WANANCHI zaidi ya 3,000 wanaoishi uwanda wa juu wa safu za Milima ya Upare wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wameingia katika mvutano kupinga ushawishi kisiasa kutaka kupindua uamuzi wa serikali wa kupandisha hadhi Zahanati ya Gojanza kuwa kituo cha afya.

Inadaiwa baadhi ya viongozi wenye ushawishi kisiasa wameingilia uamuzi huo wakishinikiza mradi wa ujenzi wa kituo cha afya ufanyike makao makuu ya Kata ya Suji, badala ya iliko zahanati hiyo Kijiji cha Gojanza.

Wakizungumza na Nipashe jana kuhusu mvutano huo, wakazi wa Gojanza, akiwamo Hawa Kituru, walidai wanachotaka kutekelezwa kwa uamuzi wa serikali wa kuiboresha zahanati hiyo ili kuepuka adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 17 kwenda ukanda wa tambarare kufuata huduma za afya katika Kituo cha Afya Makanya.

> **"Waziri wa Afya, Jenista Mhagama alipokuja hapa hivi karibuni, aliahidi serikali itatenga fedha kiasi cha milioni 600 kwa ajili ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Gojanza kuwa Kituo cha Afya.**

"Waziri wa Afya, Jenista Mhagama alipokuja hapa hivi karibuni, aliahidi serikali itatenga fedha kiasi cha milioni 600 kwa ajili ya kuipandisha hadhi Zahanati ya Gojanza kuwa Kituo cha Afya. Hao wanaotaka iende Suji hatukubaliani nao," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Konjera Elinazi alipoulizwa kuhusu mvutano huo alisema: "Wananchi wanapambana na uongozi kwa sababu tumewachangisha fedha zao, sasa wanaona kituo cha afya kinahamishwa, hawatendewi haki. Tunaomba serikali ije itusaidie hili kwa kuwa linaweza kuleta madhara hasa kwa uongozi.

Kuna watu wanaoivuruga Kata ya Suji. Maamuzi ya Ward C (Baraza la Maendeleo la Kata) yanapotolewa wao wanakuja kupangua mambo ya Ward C. Mimi kama Mwenyekiti wa Kijiji cha Gojanza, naiomba serikali ije kutusaidia kumaliza hili tatizo, vinginevyo litaleta madhara kwenye Kata hii ya Suji."

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, kumtoa mgonjwa kutoka Gojanza kumpeleka Makanya, kumesababisha madhara makubwa kiafya, hasa idadi kubwa ya wajawazito kufa njiani.

Alipotafutwa kuzungumzia mgogoro huo unaofukuta, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Yusto Mapande alithibitisha kupokea malalamiko hayo na kuahidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro huo.

"Ni kweli malalamiko yametokea kule katika Kata yetu ya Suji. Pale tuna zahanati nzuri sana ya Gojanza.

Tulipata msaada wa Serikali ya Japa, na fedha nyingine zilitolewa na Halmashauri yetu kukamilisha mradi huo, ingawa haujakamilika sawa sawa. Ilijengwa zahanati ya kisasa pale yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 300 na kitu hivi," alisema.



Baadhi ya wakazi wa Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakiangalia kibanda cha biashara kilichoteketea kwa moto juzi na kusababisha hasara. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wenye ulemavu hati hati kupata mikopo

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JAMII ya watu wenye ulemavu katika halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga hazijajengewa uwezo wa kutosha kushawishika kupata mikopo ya asilimia 10 kupitia makusanyo ya ndani, imegundulika.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, ameagiza maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri hizo kushirikiana na wadau, ikiwemo Chama cha Watu Wenye Ulemavu Tanzania (CHAWATA) kutoa elimu kuhusu mikopo hiyo ili kundi hilo likikidhi vigezo vya kunufaika na fursa hiyo.

Dk. Batilda alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na Nipashe baada ya kuzindua dirisha la mikopo hiyo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu mkoani hapa baada ya kugundua hilo.

"Mkoa wa Tanga, kuna jumla ya shilingi bilioni tisa zimetengwa kwenye halmashauri zetu zote kukuza biashara, uchumi, maendeleo na ustawi wa wanufaika na jamii kwa ujumla.

Lakini wenye ulemavu bado wako nyuma. Hawana elimu ya kutosha kuhusu mikopo hii ndio maana natamani wapate elimu bora na msaada wa karibu kuwasaidia kuwa na fursa ya kujiendeleza kiuchumi," alisema.

Julai mosi mwaka jana, serikali ilirejesha fedha za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini baada ya kusitishwa Bungeni, Dodoma Aprili 13, mwaka juzi.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, Halmashauri za Kilindi, Korogwe Mji, Lushoto, Mkinga, Pangani na Tanga Jiji, zimetoa mikopo kwa walengwa wa mpango huo.

Halmashauri za Handeni, Korogwe, Bumbuli, Muheza na Handeni Mji, ziko katika hatua za mwisho kuchakata maombi ya vikundi kwa mujibu wa taratibu kwa ajili ya kupata mikopo hiyo kwa ajili ya ujasiriamali.

# BAWASA yavuna 21m/- kwa wezi wa maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA) mkoani Manyara imekusanya Sh. milioni 12 kwa kutoza faini watu waliunganisha maji kinyemela.

Mamlaka hiyo ilibaini watu hao kujihusisha na vitendo hivyo na kuiba maji kinyume cha sheria kati ya Januari mwaka juzi na Januari mwaka jana.

Meneja Huduma kwa Wateja wa BAWASA, Rashid Charahani, alisema fedha hizo walizokusanya zimetumika kuboresha miundombinu ya maji na kununua pikipiki za mafundi ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Charahani, alisema kwa kipindi hicho matukio zaidi ya 20 ya uharibifu wa miundombinu ya maji yaliripotiwa na hatua kuchukuliwa kwa wahusika.


Alisema wanapobaini mtu ameharibu miundombinu ya maji, anatozwa faini kuanzia Sh. 500,000 mpaka Sh. milioni 50 au kifungo cha miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Kwa mujibu wa Charahani, ili kuhakikisha wizi wa maji unakomeshwa, BAWASA inatoa motisha ya Sh. 200,000 kwa mtu anayetoa taarifa hizo na za uharibifu wa miundombinu na mtoa taarifa kulindwa.

"Ofa hiyo (motisha), mtu akitoa taarifa za wizi wa maji kama ni za kweli na tukijiridhisha tunaanza kumuandalia malipo yake anayapata ndani ya siku saba na hii ni kwa wote hata watumishi wetu wote wanalipwa shilingi 200,000," alisema.

Aliyataja maeneo yaliyokithiri kwa wizi wa maji kuwa ni Katesh Mjini, Babati na Magugu.

Mkazi wa Mtaa wa Maisaka A, Adela Godwin, aliwataka BAWASA kuongeza nguvu kukagua wanaolima bustani kwa kuwa baadhi yao wanahujumu miundombinu ya maji na kuiba maji.





# Adungwa mshale wakigombea ardhi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Nhobola Wilaya ya Kishapu mkoani hapa, Musa Ngassa (39), amenusurika kifo baada ya kudungwa mshale ubavuni kwa kinachodaiwa ugomvi wa mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka mitano.

Akisimulia tukio hilo juzi katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga ambako amelazwa kwa matibabu, Ngassa alisema tukio hilo lilitokea jumatatu wiki hii majira ya jioni.

Alidai akiwa njiani akirejea nyumbani, alikutana na watu wanane miongoni mwa walioopo kwenye mgogoro nao na kushambulia kwa kipigo

Kwa mujibu wa Ngassa, wakati wakiendelea kumshambulia, mmoja kati ya hao, alimdunga kwenye ubavu wake wa kulia kwa silaha hiyo ya jadi na kumsababishia jeraha na maumivu makali.

"Kesi ilipelekwa mahakamani mimi nilishinda na nikakabidhiwa eneo hilo na Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, lakini nashangaa watu hawa bado wananiwinda na kutaka kuniua," alilalamika Ngassha.

Alidai kuwa jaribio hilo ni la nne kwa kushambuliwa na watu hao kwa lengo la kutaka kumuua ili wachukea ardhi hiyo wanayong'ang'ania kuwa ni mali yao wakati si kweli.

Alidai katika jaribio jingine la kwanza la kumuua, watu hao walimvizia na kumcharanga kwa panga kichwani na kumjeruhi.

**Dk. Dotto, alisema baada ya kufanya uchunguzi, walibaini mshale ulikuwa umeingia kwenye ini na kuutoa baada ya kumfanyia upasuaji.**

Ameviomba vyombo vya dola kuchukulia hatua kali dhidi ya watu hao ili kunusuru maisha yake kabla ya madhara makubwa hajatokea.

Dada wa majeruhi huyo, Magreth Ngasa, alisema baada ya kupata taarifa kuhusiana na tukio hilo, na watu wengine walikwenda kwenye eneo lilipotokea na kumchukua kaka yake huyo kisha kumpeleka hospitali kwa matibabu.

Daktari wa Kitengo cha Upasuaji hospitalini hapo, Dk. Matinde Dotto, alithibitisha kumpokea Ngassa akiwa katika hali mbaya huku akitokwa damu kwenye jeraha.

Dk. Dotto, alisema baada ya kufanya uchunguzi, walibaini mshale ulikuwa umeingia kwenye ini na kuutoa baada ya kumfanyia upasuaji.

Alisema hali ya majeruhi huyo inaendelea vizuri na kwamba anaweza kuruhusiwa kutoka hospitalini wakati wowote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema wanamshikilia mtu mmoja kwa tuhuma za kumjeruhi Ngassa, huku wakiendelea kuwasaka watuhumiwa wengine saba.

Magomi, alisema uchunguzi wa awali wa jeshi hilo umebaini kuwa chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa ardhi.

Ametoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kuhusiana na migogoro ili idhibitibiwe kabla ya kuleta madhara kwa jamii.



Mussa Ngassa (39) mkazi wa Kijiji cha Nhobola, wilayani Kishapu, akiwa amelazwa kwaajili ya matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga juzi, baada ya kuvamiwa na watu nane na kupigwa mshale kwenye ubavu wa kulia, wakati wakigombea ardhi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## TCRA yajivunia kukuza uchumi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imejivunia mafanikio kutokana na sekta ya mawasiliano kukuza uchumi nchini kwa kuongeza usajili wa laini za simu nchini kwa asilimia 7.7 kwa robo ya mwaka jana.

Mafanikio hayo yalitangazwa na Mkurugenzi wake wa masuala ya kisekta , Mwesigwa Felician kwenye semina kwa wahariri, waandishi na watangazaji wa vyombo vya habari Mkoa wa Mwanza kuhusu taarifa za mwenendo wa sekta ya mawasiliano kwa robo hiyo ya kuanzia Oktoba hadi Disemba mwaka jana.

Felician, alisema kwa kipindi hicho mamlaka hiyo iliongeza laini hizo kutoka milioni 80.7 za Oktoba hadi millioni 86.8 Disemba mwaka jana na kuwa hatua hiyo ni mafanikio kiuchumi kwa taifa.

Alisema ongezeko la idadi ya laini za simu zinazotumika nchini ni fursa na hatua muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia sekta ya mawasiliano.

Alisema ongezeko hilo pia ni kwa watumiaji wa huduma ya inteneti kutoka milioni 40 hadi milioni 48 huku watumiaji wa simu janja wakifikia milioni 23.

Vilevile, alisema idadi ya dakika nchini imeongezeka hadi kufikia bilioni 42.5 huku dakika kutoka nje ya nchi ikiwa bilioni 37.3 na kuwa matumizi ya intanetiyamekifikia 617 PB.

Meneja wa TCRA Kanda ya Ziwa, Imelda Banali, alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasaliano kwa Wote (UCSAF), imeanza kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo ya mipakani nchini.

Imelda, alisema hatua hiyo itatatua changamoto ya mwingiliano wa mawasiliano baina ya wakazi wa maeneo hayo na wengine nchi jirani kwa lengo la kuboresha huduma hiyo na kuchochea maendeleo katika jamii.

Hata hivyo, alisema Serikali imeweka jitihada kupitia UCSAF kuhakikisha maeneo yote ya mpakani yanafikiwa na huduma hiyo ili kuboresha usikivu wa simu, redio na kuimarisha ulinzi na usalama nchini.

# SWAT kuiwakilisha Tanzania mashindano kudhibiti ugaidi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KIKOSI Maalum cha Mbinu na Silaha nchini (SWAT) kimekabidhiwa bendera ya Taifa ya kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Vikundi Maalum vya Kupambana na Ugaidi nchini Rwanda.

Bendera hiyo ilikabidhiwa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafugwa katika Chuo cha Polisi Wanamaji Mwanza (MPC).

Akikabidhi bendera hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Polisi nchini, Camillus Wambira kwa kiongozi wa kikosi hicho, Mrakibu Msaidizi wa jeshi hilo, Isack Mwakisisile, Mutafungwa, alisema mashindano hayo yaliyoanza kufanyika jana yanatarajiwa kuhitimishwa Januari 30, mwaka huu.

Alisema mashindano hayo yatahusisha matukio matatu ya Mapambano ya Karibu, Ulengaji Shabaha na Vikwazo.

Kamanda huyo, alisema nchi 14 za ukanda wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi Ukanda wa Mashariki Mwa Afrika (EAPCCO) zinatarajiwa kushiriki katika mashindano hao.

Alisema mashindano hao yatapamba Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Majeshi ya Polisi wa Nchi za Mashariki ya Afrika (AGM) unaotarajiwa kufanyika Rwanda kuanzia Januari 27 hadi 29, mwaka huu.

Kamanda huyo, aliwasisitiza washiriki hao kuiwakilisha Tanzania vyema na kurudi na ushindi huku wakizingatia kaulimbiu ya Jeshi la Polisi nchini ' Nidhamu, Haki, Weledi na Uadilifu'.

Mbali na kuwatakia kila la heri, Mutafugwa aliwahimiza kujituma zaidi kwani hakuna mafanikio bila kufanya hivyo na kuongeza ushirikiano miongoni mwao na washiriki wengine.

"Jeshi la Polisi ni taasisi kubwa na limejijengea heshima kubwa ndani na nje ya nchi, sisi hatuna wasiwasi tunatarajia kuona mnarudi na ushindi, hivyo mnatakiwa kuongeza morari" alisema.

Mkuu wa msafara wa kikosi hicho, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Isack Mwakisisile, alisema wamejiandaa vizuri na wanamatumaini makubwa ya kurejea nchini wakiwa na ushindi.




Ukurasa 13

Tunaendekeza sana lugha, utamaduni wa kigeni!




**Namna Mchungaji alivyowafunda kinamama waliotoka vifungoni maisha mapya ya uchumi wenye busara**

Ukurasa 12


# BUFE

IJUMAA JANUARI 24, 2025

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


BAADA MKUTANO NISHATI DAR...

# Bashe: Samia mwenyeji tena Februari walima zao la kahawa Afrika kujadili 'utakavyowatoa'

## •Adokeza ushindi ajira, hadi biashara ijavyo nchini

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MWEZI ujao Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Tatu wa Nchi zinazozalisha Kahawa Afrika (G25 African Coffee Summit), unaoandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Kahawa la Afrika (IACO).

Ni mkutano uliopangwa kufanyika kati ya Februari 21 hadi 22, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) kilichopo Dar es Salaam, huku kauli mbiu ya mkutano huo ikiwa ni "Kufungua Fursa za Ajira kwa Vijana Kupitia Uboreshaji wa Sekta ya Kahawa Afrika."

Katika mkutano huo, ambao mgeni rasmi anatarajia kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, utahudhuriwa na Wakuu wa nchi zinazolima kahawa barani Afrika, mawaziri wa kilimo, sekta binafsi, viongozi wa taasisi za kahawa katika nchi zinazolima kahawa,wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la kahawa.

Ni mkutano unaofanyika wiki nne, baada ya kufanyika tukio kubwa kama hilo kwa ngazi hiyo barani Afrika katika ukumbui huo tajwa, nao ukichukua siku mbili, wenyewe ukihusu sekta nishati, Rais Dk. Samia, naye akiwa mwenyeji wao.

Ni mkutano unaotarajiwa kutoa mwongozo wa jinsi ya kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU), mashirika yake, benki za maendeleo za Afrika na taasisi nyinginezo za fedha, ili kuunda programu zinazochochea ujasiriamali na ajira kwa vijana kupitia sekta ya kahawa.




Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati) akishika kitufe jijini Dodoma, kuashiria kuanza kwa maandalizi ya Mkutano wa Tatu wa Nchi 25 za Afrika zinazozalisha Kahawa (G25).Wa kwanza kushoto, ni Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde. **PICHA:RENATHA MSUNGU**

Katika Mkutano huo wa Tatu wa kahawa, kutajadiliwa maeneo muhimu katika mnyororo wa thamani wa kahawa, kufungua fursa za biashara na ajira kwa vijana katika maeneo mbalimbali.

Mkutano huo unaoshirikisha nchi 25 zinazolima kahawa Afrika, ni wa kuongeza ujuzi kuhusiana na zao hilo, kupata usahihi wa mnyororo wa thamani wa zao hilo.

**WAZIRI WA KILIMO**

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe anasema utekelezaji kiserikali, umeshaanza kupitia wizara yake, wakizindua programu ya ujasiriamali kwa vijana iitwayo 'Jenga Kesho Iliyo Bora' (Build a Better Tomorrow - BBT).

Katika hilo, ina maudhui ya mipango inayotekelezwa ni kuanzisha wanachokiita "maduka ya kahawa yanayotembea," kwa lengo la kuchochea na kuongeza matumizi ya kahawa nchini.

Bashe anasema, ni migahawa itakayowezesha vijana wajasiriamali kujiajiri katika maeneo mbalimbali, ikiwamo barabarani na kwenye matukio ya umma katika maisha ya kijamii.

Pia, Bashe anasema pindi mkutano huo utakapoisha, utawasaidia vijana kuanzisha vituo mahiri vya kuuza kahawa, kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu, ili kuelimisha vijana mnyororo wa thamani wa kahawa, kutoka uzalishaji hadi matumizi.

Anafafanua, kuwa ni mpango unaoanzisha kikao cha wazalishaji kahawa Afrika, ni matokeo ya azimio lililopitishwa katika Mkutano wa 61 wa Mwaka wa IACO uliofanyika Kigali, Rwanda, Novemba 18, 2021.

Inatajwa ililenga kuandaa mkutano wa ngazi ya juu wa nchi 25 zinazozalisha kahawa Afrika, ili kutathmini mapungufu na changamoto zinazodumaza sekta hiyo katika ukanda huo.

Anasema, katika mkutano wa kwanza wa nchi hizo wazalishaji kahawa, ulifanyika nchini Kenya mnamo Mei 2022, ulipitisha kinachoitwa "Tamko la Nairobi"(Nairobi Declaration).

Hilo liliazimia kuweka mkakati wa kuingiza kahawa, kuwa bidhaa muhimu ya kimkakati ndani ya AU, sambamba na ajenda mwaka 2063 kwa AU.

Anasema mkutano wa pili wa nchi wazalishaji kahawa Afrika, ulifanyika Kampala, Uganda, Agosti mwaka 2023, ulipitisha

Inaendelea Uk 14

UCHUMI

# Namna Mchungaji alivyowafunda kinamama waliotoka vifungoni maisha mapya ya uchumi wenye busara

**Na Beatrice Philemon**

INAPOZUNGUMZIWA kanuni zinazomsaidia mtu kuwa na uchumi imara katika maisha yake, si wote wanaozifahamu.

Ili mtu aweze kufanikiwa kiuchumi, iwe binafsi au kwa biashara, anatakiwa kuzingatia kanuni zifuatazo:

Hizo zinajumuisha kubadilisha mtazamo na mawazo yanayohusiana na dhana mafanikio, kukiwapo maono au ndoto chanya, zikiguswa na kufanya kazi kwa bidii, ubora na uaminifu.

Vilevile, kuna maoni yanayogusa maeneo: Nidhamu ya fedha na kubana matumizi; kuwa na utamaduni wa kuweka akiba; na kujiepushe na madeni.

Pia, kukaongezwa dhana ya kutunza afya ambayo ni mtaji mkubwa sana katika kufanikiwa afya na uhai, analitaja mshauri huyo kuwa suala la baraka kuu kiimani, pasipo kusahauliwa mahitaji ya kibinadamu.

Hapo yanaorodhesha mazoezi ya mwili; kunywa na kula, pia kupata mwanga wa jua, kuvuta hewa safi, pia kupumzika.

Mchungaji Lucas Mwimo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa Tanzania Prisoners Hope Foundation (TPHP), ametamka hayo katika mazungumzo na wanawake waliomaliza vifungo magerezani.

Mchungaji Mwimo, akawaasa kuepuka tamaa, hasa wanapoona uchumi wako umeanguka au hauendi vizuri.

"Hofu ni mlango ambao adui au shetani anautumia ili kumtesa mwanadamu, hofu huondoa tumaini na nguvu ya imani, kwa hiyo jitahidi kukataa hofu na kukata tamaa," anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Prisoners Hope Foundation (TPHP), Mchungaji Lucas Mwimo, akiwa darasani, Mbweni, Dar es Salaam, kuwanoa kiuchumi kinamama waliomaliza vifungo magerezani. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

**KANUNI YA KWANZA**

Inatajwa kuwa ili mtu abadilishe mitazamo kwa mtazamo wake, kuhusu dhana ya mafanikio.

Mitazamo inarejewa kuwa picha ya ndani ya mtu kuhusu jambo fulani, kutokana na mawazo na maamuzi yanayofanya kila siku yakitafsiri kushinda au kushindwa kimaisha.

Mwimo anaeleza: "Aina ya mawazo na mtazamo inaamua hatima ya maisha utakayoishi, ama maisha ya juu, kawaida au umaskini.

"Jitahidi kukataa mawazo ya kinyonge na mtazamo mbaya wa kushindwa. Ukitaka kufanikiwa na kuwa na uchumi bora, shikilia mtazamo wa ushindi, utele na utajiri katika mawazo yako."

**KANUNI YA PILI**

Maono anayataja kuwa picha ya ndani kimaisha, mtu anataka ama kuishi nayo au walau kuyafikia, ngazi ya nafsi au maisha mtu anataka kuyafikia baadaye.

Anataja hatua kuu ya kwanza, ni kujiwekea maono binafsi, akiwa na ufafanuzi kwamba asiye na maono, daima anakosa mafanikio, kila mtu aliyefanikiwa alianza kwa maono.

"Jitahidi uwe na picha ya maisha yako, jitahidi upajue unapokwenda na hapo yalipo maisha na mafanikio yako, moja ya sifa za watu wakuu waliofanya makubwa duniani na kuacha alama ni maisha ya maono," anasema.

**FAIDA YA MAONO**

Kuna maono yanayompa mtu uwajibikaji na kuukomboa wakati, yanampa nidhamu.

Mwimo anasema kwamba kila mwenye maono, ni lazima kujiwekea nidhamu ya nini cha kufanya na nini cha kutofanya ili kufikia ndoto yake.

Pia, anatetea maono kwamba, huamua mtu anakopaswa kupafikia, akinena kanuni ni mtu ana nafasi ya kufikia anakopabashiri, yakimpa lengo na kujiandaa vizuri kuyatekeleza.

**BIDII, UBORA NA UAMINIFU**

Mwimo anasema, fedha na utajiri hupatikana kupitia kufanya kazi na shughuli halali za kiuchumi.

"Ili ufanikiwe, fanya kazi au biashara na shughuli za kiuchumi kwa bidii na kwa uaminifu. Hakuna aliyefanikiwa katika maisha bila ya kufanya kazi kwa bidii..." anatamka Mchungaji Mwimo.

"Tusifanye kazi bora liende, bali kwa ubora. Kitakachokupa wateja na kibali ni ubora wa bidhaa unazozalisha, pia kitakachokupa 'promosheni' kazini, ni ubora wa kazi unazozifanya!" anasema

**KANUNI BORA KIBIASHARA**

Mwimo anataja biashara ni kazi za kuinua uchumi, hasa inapofanywa kwa kufuata kanuni za kiuchumi na biashara.

Baadhi ya kanuni za kufanikisha biashara yako ni kama: Kufanya utafiti wa kutosha na kujiridhisha biashara hiyo inaleta faida.

Pia, Mwimo akaeleza kuwapo soko au wateja wa kudumu wa kununua bidhaa au huduma, huku akitaja biashara ni kitu muhimu, hasa inapokuwa katika sehemu nzuri.

Kwa biashara za rejareja, kunatajwa panafaa mahali penye watu wengi wanakopita, wakichagua fursa au masoko na mauzo ya jumla.

Anataja kanuni nyingine ni kuwapo muuzaji makini, mchangamfu na anayesikiliza na kuwajali wateja, ikiendana na analolitaja kuwa suala la 'Mteja ni Mfalme.'

Hapo Mchungaji Mwimo ana ufafanuzi wake kuwa:"Hii itasaidia kujenga uhusiano mzuri kati yako na wateja wako.

"Ni lazima uwashawishi, kwanini waje kununua kwako na sio kwa wengine, pia usafi wa mazingira ya biashara na usafi wa muuzaji."

Pia, wanasisitizwa wahusika kutouza vitu viliyokwisha muda wake (vyakula), mbadala wake kuwekewa vivutio mbalimbali, kama vile kupunguza bei kwa baadhi ya vitu.

Hiyo anaitaja inaendana na kuwapo matangazo ya utambulisho wa biashara kuwavutia wateja, pia ukopeshaji kwa wateja waaminifu.

Vilevile inaendana na biashara hiyo ikifunguliwa kwa wakati sahihi, hakuna kauli za hasira kwa wateja na ina hamasa

"Kwa mfano. kama wateja wanaulizia bidhaa hiyo hiyo na wewe hunayo, nenda ukaitafute," anasema Mwimo.

Eneo lingine linatajwa, ni kuweka aina nyingi za bidhaa kumuwezesha mnunuzi anunue vitu mahali, pamoja, huku wenye biashara kiserikali na sekta nyinginezo zinazomhusu, akiwajibika kulipa kodi.

Hapo inaendana na kuwapo daftari lake la kutunza hesabu inayomhusu.

**KANUNI YA NNE NIDHAMU YA FEDHA NA KUBANA MATUMIZI**

Mafanikio ya kiuchumi/biashara yanahitaji nidhamu ya fedha na matumizi, kinachofanya watu wengi washindwe kufikia ndoto za mafanikio ya uchumi na maisha yao ni tatizo la matumizi mabaya ya fedha yasiyo na nidhamu.

Anasema, sababu kubwa ya watu kutoweka akiba ni kutodhibiti matumizi na ukishaweza kujizuia kwenye matumizi, tegemea utajiri.

"Matumizi ndiyo yanayoamua hatima ya utajiri au umaskini, umaskini ni hali ya matumizi yako kuwa makubwa kuliko kipato chako, jifunze kuweka vipaumbele juu ya mahitaji muhimu utakayo fanya kwa pesa iliyopo mkononi mwako na usijaribu kutaka kutekeleza kila hitaji," anasema

Anasema, mahitaji ni mengi hutaweza kuyamaliza, michango ni mingi hutaweza kumchangia kila mtu, kukiwapo maisha ya uhalisia na kuepuka matumizi ya fedha.

Hiyo inatajwa, ili kuwaridhisha wanadamu pamoja na ndugu zako na moja ya kitu kitakachokusaidia kuwa na matumizi mazuri ni kuandaa bajeti na kuiheshimu.

**MAANA YA BAJETI**

Bajeti maana yake ni kuoanisha mapato na matumizi, kupanga na kutawala matumizi, kupanga bajeti ni kwa muhimu kama vile ilivyo muhimu kufanya kazi, bajeti inayofanikiwa ni lazima izingatie mambo yafuatayo:

Bajeti ni lazima itokane na mapato na sio mategemeo, lazima iwe ya kweli na ya utaratibu, fedha ni lazima zipangwe kulingana na hitaji la kweli, mume na mke ni budi wafanye pamoja kufanikisha bajeti yao.

"Bajeti inaweza kuwa ya wiki au ya mwezi kutegemeana na vyanzo vya mapato, bajeti yenye mafanikio inahitaji utaratibu wa kutunza mahesabu.

"Hiyo ni kama vile, kuwa na kitabu cha bajeti kuandika manunuzi yote, au bahasha zinazofichwa kwa usalama zenye fedha zote zilizopangwa...," anasema

Pia, anataja, penye mapato yasiyoendana na uhalisia wa mahitaji, inapaswa kufanyiwa marekebisho ama kwa kupata mapato zaidi au kuyapunguza.

**KUWEKA AKIBA**

Anasema lengo la kuweka akiba, ni kupata fedha za dharura, ili kujiepusha na mikopo isiyokuwa ya lazima na kupata fedha ya mtaji kwa ajili ya uwekezaji.

Pia, anafafanua kuwa mtu anatakiwa kuweka akiba kwa kila fedha unayoipata na kuiweka kwenye akaunti kwenye benki, kibubu, au simu, kila fedha inayoingia mikononi mwako ina mkate na mbegu (Akiba).

Pia, kunatajwa kuwapo watu waliofanikiwa sana katika maisha na wamejitahidi kujinyima, hata kujijengea mazoea ya kuweka akiba kwa awamu.

Mwimo anaendelea kuwaasa: "Tofauti ya masikini na tajiri ni kwamba maskini akipata pesa anakula kwanza kisha anawekeza kama itakuwa imebakia.

"Tajiri akipata pesa, anawekeza kwanza, kisha anakula inayobaki. Hakuna tajiri asiyeweka akiba. Mweka akiba yupo kwenye njia ya utajiri," anafafanua katika mada yake.

Hapo anawaasa kinamama hao, kujenga tabia ya kutenga akiba kabla ya matumizi, mathalan asimilia 10 ya mapato ni hali inayomkingia mtu adha ya madeni yasiyo ya lazima, kwani asiyeweka akiba hawezi kukwepa madeni.

Hapo anawapa kanuni kwamba, "adui mkubwa wa kuweka akiba ni kuahirisha" na wito wake ni kwao kuanza hilo mara moja.

**KANUNI YA SITA**

Hatua hiyo, anawasisitizia kuepuka madeni na mikopo pale inapobidi au hakuna ulazima wake, isipokuwa katika ulazima au dharura. Mtazamo ni kwamba 'madeni sio dhambi, ila ni mzigo na utumwa unaotunyima pumziko.




Namna darasa la waliotoka gerezani lilivyoendelea.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tunaendekeza sana lugha, hata utamaduni wa kigeni!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

KATIKA historia, kuna marehemu wawili huwakumbuka sana kutokana na misimamo yao ya kujitambua na hasa kutambua asili yao; mmoja Mwafrika na mwingine ni Mmarekani mwenye asili ya Afrika.

Mwafrika, kiongozi wa nchi aliyejulikana kama Mobutu na Mmarekani ni mwanamichezo mwanamasumbwi aliyeibuka kinara duniani na si mwingine, bali ni Muhammad.

Huyu Mobutu alizaliwa akiitwa jina la Joseph Desire na wazazi wake, baba yake akiitwa Mobutu. Lakini, baadaye akaona isiwe taabu, alipopata uraisi wa nchi iliyokuwa ikiitwa Congo, akabadili jina lake na la nchi.

Yeye akajiita Mobutu Sese Seko Kuku Ng'bendu wa Zabanga, huku nchi yake akiibadili jina na kuiita Zaire, akikataa kuitwa majina yaliyotoka kwa wageni waliokuja kututawala kwa maslahi yao binafsi, hivyo kutaka kutuvika utamaduni wao na wakafanikiwa.

Marekani akawapo manamsumbwi aliyejulikana kwa jina la Cassius Clay, jina la Wazungu hilo, akabadili na kusilimu akachukua jina la Muhammad Ali, ingawa si la kiafrika kwa asili, lakini angalau alikataa kasumba ya kigeni na kuendana na hili linalokubalika hata kwa Waafrika.

Wazaire walimwunga mkono Mobutu kwa kasi ya ajabu na karibu kila mmoja akakataa jina la kigeni na kubaki na la kikongo, hadi alipoingia madarakani Laurent Desire Kabila na ghafla Zaire ikawa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Waendelee kupumzika pema Mobutu na Muhammad!

Athari hasi hizi zimetamalaki katika mataifa mengi ya Kiafrika hasa yaliyotawaliwa na wageni hao, ambako majina ya Waafrika si ya kijadi tena, bali ya wageni, ingawa kuna baadhi ya makabila katika mataifa hayo, yameendelea kusimama kwenye majina yao ya asili.

Nchini mathalan, Wahadzabe wanastahili kuvuliwa kofia kwa kushikilia utamaduni wao, ingawa kuna wengine wanatakiwa kuelimishwa waachane nayo, ikiwa ni pamoja na ulaji nyama mbichi, pia kuchukulia kuoga ni kama anasa kwao. Yawezekana ni utamaduni, lakini uko hasi!

Nchini, tuko mstari wa mbele sana kujitapa na kujimwambafai, kuwa tunapigania na kudumisha utamaduni wetu, lakini kuna baadhi yetu imebaki kuwa nadharia isiyo kwenye vitendo, kwani tunashuhudia jinsi baadhi wanavyojisika anapolinganishwa au kufananishwa na kuwa wa jamii za mataifa hayo makubwa yaliyopiga hatua.

Chukulia mbongo utakayeonana naye mchana akiwa njiani kwenda baa, utazungumza naye Kiswahili kizuri mkaelewana, lakini akishakalia kigoda akaanza chupa ya kwanza, ya pili na kukaribia ya 10, Kiswahili kwishney, hajui tena, sasa anazungumza Kiingereza hata kama kibovu.

Tunashuhudia baadhi ya watangazaji wetu kwenye vyombo vyetu vya habari wakijadili mambo, hatawakosa kuchanganya na Kiingereza, ili mradi kujitanabahisha kuelewa somo vizuri, ingawa pia Kiingereza hicho ni tiamaji-tiamaji.

Huku kwenye majina ndiko usiseme, mtu anazaliwa na jina lake zuri tu na kusajiliwa kwenye cheti cha kuzaliwa, akipata elimu kidogo na pengine akaibuka nyota katika jambo fulani, hilo jina alilopewa na wazazi atalisigina na kuibuka na lingine angalau la Kizungu.

Wapo wanaojiita majina ya madini, ili mradi kuonekana wanang'ara na mbaya zaidi hata kujitambulisha rasmi wakitumia majina yasiyo rasmi kwenye vyeti vyao vya kuzaliwa au vitambulisho vya Nida! Huku kote ni kukanyaga asili na utamaduni! Kwani ukijiita jina la gari inakusaidia nini?

Tupo tunaojitapa sana kuenzi utamaduni na hasa lugha yetu, lakini hebu tazama vituo vingi vya habari hasa vya kielektroniki, vinavyotangaza kwa Kiswahili, vina mambo mengi ya kigeni wanavyorusha!

Hivi karibuni, sekta ya habari imepata Waziri mpya pia ni mwanahabari, Profesa Palamagamba Kabudi, ambaye anajinasibisha na kuhakikisha lugha fasaha ya Kiswahili inatumika katika kuwasilisha ujumbe na elimu kwa umma.

Namhurumia sana Profesa, kwamba anajitahidi sana, ila mafanikio ya hilo analotaka nahisi yako mbali, kwa sababu hivi sasa vyombo vyake vya habari vimejaa wasanii wasio na elimu ya lugha, bali kutangaza lolote linalowajia.

Tunahitaji mapinduzi makubwa katika kuhakikisha tunaendeleza Kiswahili fasaha, hasa kwa kuzingatia kuwa sisi ndilo chimbuko la lugha hiyo, lakini kuna kasoro za waendehaji vipindi.

Kwa namna hiyo, tuendako safari itakuwa ndefu sana, gari kuzimikia njiani. Tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa, titi hili la mama ambalo ni tamu, linaendelea kutupa maziwa kwani hatuna kwingine kwa kunyonya, bali hapa hapa nyumbani.

Tumwunge mkono Profesa Kabudi, huenda akatuvusha kutoka tope hili la uchafuzi wa lugha na utamaduni. Nilikuwapo!

## BIASHARA

# Soko jipya Tandale kuingizia manispaa Mil. 912/- kila mwaka, kilio ni wafikiwe

## • RAS Dar aagiza wafuatwe LATRA kufikike

**Na Sabato Kasika**

HIVI sasa kuna mradi wa ujenzi wa soko la kisasa la Tandale uliopo Dar es Salaam, ambao ni wa kimkakati, kukitarajiwa kuingizia Halmashauri ya Wilaya Kinondoni Sh. milioni 2.5 kila siku.

Hiyo ni sawa na Sh. milioni 75 kila mwezi, vivyo hivyo wastani wa shilingi milioni 912 kila mwaka.

Kimsingi, ujenzi wa soko hilo wenye thamani ya Sh. bilioni 10.2, ulianza mwaka 2013, kwa fedha kutoka serikali kuu, sasa wafanyabiashara waameanza kulitumia, huku taratibu za kulizindua rasmi ukiandaliwa.

Wafanyabiashara wa soko hilo lililojengwa kisasa likiwa na ghorofa mbili walianza kuingia ndani Oktoba mwaka jana na sasa wanaendelea na biashara zao kama kawaida.

"Soko lilikamilika na kuanza kazi rasmi, litakuwa linaiingizia Manispaa ya Kinondoni mapato ya Sh. milioni 2.5 kwa siku," anatamka Mweka Hazina wa Manispaa Kinodoni,' Onesmo Mwonga.

Anafafanua hayo, katika ziara ya Katibu Tawala wa mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Toba Nguvila, hivi karibuni alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wake.

Katika maelezo yake ni kwamba, soko hilo lina vitengo mbalimbali ambavyo manispaa itaweze kukusanya Sh. milioni 2.5 kila siku kutoka kwa wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao humo.



Soko la Tandale, katika Manispaa ya Kinondoni, likiwa katika hatua ya ujenzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Anafafanua kuwa, ujenzi wa soko hilo umefikia asilimia 99 na kwamba utaratibu wa kupanga wafanyabiashara umefanywa kwa kuzingatia mahitaji ya kila mfanyabiashara na aina ya bidhaa wanazouza.

Ofisa Biashara, Viwanda na Uwekezaji wa Manispaa Kinondoni, Phillipo Mwakibete, anasema matarajio ya manispaa ni kuona wafanyabiashara wote wakinufaika na fursa hiyo ya kuwa na soko la kisasa.

"Soko litawezesha wafanyabiashara kuuza bidhaa zao katika mazingira safi na salama, na kwamba soko la hilo lina zaidi ya wafanyabiashara 2000 wa vitendo mbalimbali wakiwamo mama lishe na baba lishe.

**CHANGAMOTO**

Mwenyekiti wa soko hilo, Sultan Kiumbo, anasema pamoja na hatua zilizochukuliwa na manispaa kuliboresha kuwa la kisasa, bado kuna changamoto inayowakabili.

Kiumbo anaitaja kuwa, ni ukosefu wa usafiri wa daladala za kufika sokoni hapo, hali inayosababisha wateja kwenda katika masoko mengine, ambayo yanafikika kirahisi.

"Soko letu liko maeneo ya katikati ya Tandale, hakuna daladala zinazofika hapa, bali zinashusha abiria kwa Mtogole Kwa Tumbo (Barabara kuu ya Magomeni- Sinza), au Manzese Argentina (Barabara Morogoro) ambako ni mbali halafu njiani kuna vibaka, hivyo wateja wanaohofia usalama wao," anasema Kiumbo.

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, muda wa wateja kufuata bidhaa sokoni huwa ni alfajiri na kwamba muda huo ndio ambao pia 'vibaka' huwinda watu kuwapora mali zao.

"Katika mazingira hayo, ni vigumu mteja kushuka Kwa Mtogole, Kwa Tumbo au Argentina afajiri ili afuate bidhaa Tandale, badala yake anakwenda soko lingine kwa ajili ya usalama wake," anasema.

Kiumbo anasema anatamani soko hilo liwe kama masoko ya Temeke, Simu 2000, Mabibo na mengine ambayo yanafikika kirahisi wakati wote bila usumbufu wala hofu kwa wateja.

Anasema sio vibaya daladala zikawa zinashuka abiri na kuendelea na safari za kwenda katikati ya jiji, Ubungo, Mabibo, Makumbusho na maeneo mengine ili iwe rahisi kwa wateja kufika sokoni hapo.

"Soko letu lina vitengo vingi vikiwamo vya mazao ya nafasi, mama lishe na baba lishe, viazi vitamu, viazi mviringo, nafaka, mihogo, miwa na vingine vingi vinavyoweza kuingizia manispaa mapato ya kutosha, kwani ushuru ukiwaamo unaoanzia shilingi 500 kwa siku," anasema.

**MAAGIZO YA RAS**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Toba Nguvila, anamuagiza Katibu Tawala wa Manispaa ya Kinondoni na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, kukutana na viongozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kupanga 'ruti' za kufika sokoni hapo.

Dk. Nguvila anatamka kuwa, changamoto mbalimbali zilizopo sokoni hapo zitatuliwe haraka ikiwamo pia kuboresha mfumo na vyoo ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara.

Anafafanua kuwa lengo ni kuhakikisha wafanyabiashara wanaendesha shughuli zao bila usumbufu, huku wateja wao nao wakija kupata huduma bila kikwazo chochote hasa kwa upande wa usafiri.

Kiongozi huyo anaongeza kuwa kuna haja ya soko kuwa ua jenereta kubwa ambalo litasaidia biashara kufanyika muda wote bila usumbufu wa ukosefu wa umeme, kwa kuwa ni soko la kisasa.

"Wito wangu ni kwamba kusiwe na kero au changamoto zozote zikiwamo za mafuriko wakati wa mvua, badala yake kazi ifanyike kuhakikisha soko linafanya kazi kwa ufanisi.," anasema Dk. Nguvila.

# BASHE: SAMIA MWENYEJI TENA FEBRUARI WALIMA KAHAWA AFRIKA KUJADILI 'UTAKAVYOWATOA' KIUCHUMI

Inatoka Uk 11

tamko lililokusudia kuwaomba wakuu wa nchi 25 wazalisha kahawa kuunga mkono uidhinishaji kuwa bidhaa muhimu ya mkakati katika Ajenda ya AU mwaka 2063 na kuifanya IACO, kuwa shirika maalum la umoja huo.

Bashe anasema, katika kikao cha Baraza Kuu la AU, Februari mwaka jana huko Addis Ababa, wakuu wa nchi na serikali waliridhia ombi hilo; kahawa kuwa bidhaa muhimu katika mkakati na ajenda ya AU, mwaka 2063 ya AU, pia IACO kuwa shirika lake maalum.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA NCHINI**

Bashe anataja hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto za biashara ya kahawa, baina ya nchi za Afrika, ni kuanzishwa Mkataba wa Biashara Huria Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA) wa mwaka 2018.

Anasema, lengo ni kuondoa vikwazo vya biashara katika nchi za Afrika, ili utekelezaji wa mkataba huo uimarishe biashara ya kahawa pasipo vizuizi.

**USHIRIKI WA VIJANA**

Carloline Samson, ni mjasiriamali mdogo, anataja faida kubwa ya mkutano ni jamii kujua umuhimu wa zao hilo la biashara na mnyororo wa thamani.

Anaipongeza serikali kwa kuandaa mkutano huo, akiamini utawaondolea kasoro ya ajira, hata wakajiajiri kupitia biashara ndogo za bidhaa hiyo, katika maeneo mbalimbali.

Anataja mkutano mkubwa wa ngazi hiyo, utawatambulisha wakulima wa kahawa wa nchini, pia kutatoa fursa kwa vijana kupata uzoefu kutoka kwa wakulima wakubwa wa zao hilo kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi.

Caroline anasema serikali hivi sasa imewekeza katika sekta ya kilimo, hivyo mikutano mikubwa kama hiyo, inawasaidia kufungua fursa mbalimbali ambazo zinawasaidia vijana kujiinua kiuchumi wao wenyewe na familia zao.

Mjasiriamali huyo, anaishukuru Wizara ya Kilimo kwa ubunifu wa miradi itokanayo na sekta kilimo, ikiwasaidia vijana kujikwamua kiuchumi, katika maeneo mbalimbali.

Mwigine ni Tito Mathiasa, anayesema kilimo cha sasa kinazidi kuhamia katika mapinduzi teknolojia, hivyo serikali kukubali kuandaa mkutano huo ni ya fursa ya kuwakutanisha wadau wa kahawa pamoja, kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali yanayohusu kilimo cha kahawa pamoja na mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Tito anaeleza kuwa, mkutano huo utatoa fursa nyingi kwa wakulima wa zao la kahawa, pia kupanua wigo wa kilimo cha kahawa nchini, ikiwamo kubadilishana mawazo wafanyabiashara na wazalishaji wa zao hilo la kahawa.

**WADAU KILIMO KAHAWA**

Mkulima Joshua Maganza, anasema mkutano huo ujao wa kahawa, utazidi kuitambulisha nchi kwenye kilimo hicho duniani, pia utazidi kuwashawishi wakulima kutanua wigo wa kilimo hicho nchini.

Anasema Wizara ya Kilimo, pamoja na serikali kwa ujumla, wako katika kukuza mazao ya kimkakati kama kahawa, jambo linalosaidia kuwashawishi wakulima kuongeza idadi ya ukubwa wa mashamba yao.

Anahimiza umuhimu wa zao la kahawa, pia kuwa la kimkakati, ambalo mkulima akifuata taratibu za kitaalamu za uandaaji wake, inapanua kiwango cha uzalishaji, hata kuongeza kipato cha familia.



## HABARI DODOMA

# Watumishi wanaokwamisha walimu kukiona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na watu wenye ulemavu imesisitiza itaendelea kuwachukulia hatua kali watumishi wa umma ambao ni kikwazo kwa walimu nchini kutatua kero zao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wake, Patrobasi Katambi wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Walimu Wanawake Taifa.

Katambi, alisema serikali itahakikisha watumishi hao ambao wanachukuliwa hatua za kinidhamu kwa kusababisha walimu nchini kushindwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Aliipongeza CWT kwa utulivu uliopo na kwa namna viongozi wake wanavyokiendesha chama hicho na kutatua kero zinazowakabili walimu katika maeneo mengi nchini.

Makamu wa Rais wa CWT, Suleiman Ikomba, alisema licha ya jitihada za serikali kutatua kero zinazowakabili walimu, kuna watumishi wa umma wameshindwa kutumiza majukumu yao. Ikomba, alisema watumishi hao waliokabidhiwa dhamana ya kuwahudumia walimu wameshindwa kutimiza wajibu wao.

"Tunaipongeza sana serikali yetu chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akitatua changamoto zinazowakabili walimu ikiwemo malimbikizo ya madeni ya mishahara na likizo.

"Mwalimu mmoja anaweza akawa anafundishi wanafunzi 200,kama kero yake haitatimiziwa katika eneo alipo na kutoka kufuata mkoa mwingine anaathiri ufundishaji wa wanafunzi kwa muda wote ambao hakuwepo katika kituo chake cha kazi, "alisema.

Katibu Mkuu wa CWT, Joseph Misalaba, alisema CWT aliipongeza serikali kwa kwa kutumia kliniki tembezi ya kutatua kero zinazowakabili walimu nchini.



Katibu wa Bunge ambaye pia ni Katibu wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, Baraka Leonard (kulia), akizungumza na Mwenyekiti wa Makatibu Mezani wa Chama hicho na Katibu wa Bunge la Sierra Leone, Paran Tarawally (kushoto), alipomtembelea ofisini kwake, Bungeni jijini Dodoma, jana. Katikati ni Makamu Mwenyekiti wa Makatibu Mezani wa Chama hicho na Katibu wa Bunge la Malawi, Fiona Kalemba. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Serikali yajizatiti ufugaji samaki kwa vizimba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI itaendelea kuimarisha miradi ya ukuzaji viumbe maji kwa njia ya vizimba vya kufugia samaki nchini ili kuongeza uzalishaji wa samaki, uchumi wa wananchi na taifa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji, Dk. Nazael Madalla kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika mkutano wa kujadili kuimarisha Tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji kwa vizimba kwa kushirikiana na

Shirika la Uhifadhi wa Mazingira la The Nature Conservancy (TNC) na taasisi za serikali na binafsi.

Dk. Masala, alisema hatua hiyo inafuatia Rais Samia Suluhu Hassan kuelekeza wizara hiyo kuhamasisha ufugaji samaki kwa vizimba ili kuongoza uzalisaji wa kitoweo hicho, kutoa ajira kwa vijana nchini na kukuza uchumi wa taifa. Alisema Ziwa Tanganyika ni moja ya maeneo nchini yenye fursa ya ufugaji samaki kwa njia hiyo, hivyo wamekutana na wadau kutoka ndani na nje ya nchi kuweka mikakati ya kuhakikisha kunakuwa na uwezeshaji, ulinzi wa mazingira na utunzaji vizimba hivyo ili viwe endelevu. "Tunafanya hivyo ili kuhakikisha wafugaji samaki wanufaika pamoja na taifa katika Sekta ya Ufugaji Samaki Kwa njia ya Vizimba," alisema Dk. Madalla.

Alisema serikali imekuwa ikifanya juhudi kukuza tasnia hiyo ya ukuzaji viumbe majini kwa kupeleka vizimba katika ziwa hilo na kufanya ziara kuhakikisha mpango huo unafanikiwa kwa manufaa ya jamii na taifa.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa wavuvi ya ufugaji huo na mikopo ya pembejeo ili kuendeleza maeneo hayo ya mkakati.

"Lengo la serikali ni kuanza taratibu za kuanzisha Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Ziwa Tanganyika, kuhamasisha jamii na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji," alisema Madalla

Akizungumzia kuhusu mwitikio wa wananchi kufuga samaki kwa vizimba, alisema umeanza kuongezeka kutokana na serikali kuweka mazingira rafiki, kutoa mikopo na kuwanufaisha wafugaji wengi. Mkurugenzi wa Uvuvi wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (LTA), Nyakorema Marwa, alisema mafunzo hayo yameshirikisha wadau wa tasnia hiyo wa taasisi za serikali na binafsi kuandaa mpango wa utekelezaji usiokinzana na sheria za nchi nne zinazozunguka ziwa hilo.

Meneja wa Mradi wa Ziwa Tanganyika wa TNC, Fridolin Nzambimana, allisema wanachokifanya ni kuimarisha ushirikiano baina yao, serikali na taasisi nyingine ili kukuza tasnia ya ukuzaji viumbe maji kwa vizimba na kulinda rasilimali za uvuvi.

# Wabunge wapongeza ustawi, maendeleo nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeipongeza Serikali kwa kuimarisha ustawi na maendeleo ya Watanzania katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq wakati akihitimisha kikao cha Kamati hiyo na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Bungeni jijini hapa juzi.

Kikao hicho kilikuwa maalum kwa ajili ya ofisi hiyo na taasisi zake kuwasilisha taarifa ya utendaji kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba, mwaka jana

"NSSF, OSHA, WCF na CMA kwa kweli kazi mnazofanya zinaonekana pamoja na changamoto chache zilizopo, sisi kama kamati tunaridhika na jinsi mnavyotekeleza majukumu yenu," alisema na kuongeza kuwa:

"Kwa namna ya pekee nimpongeze Rais wetu, Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake makini kwani tunatambua dhima kuu ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kunakua na ustawi na maendeleo ya Watanzania hususan wafanyakazi katika sekta rasmi na isiyo rasmi."

Mwenyekiti huyo wa kamati, alisema nia njema ya Rais Samia kuboresha ustawi wa wananchi wake inajidhihirisha katika jitihada ambazo serikali yake imekua ikichukua kuimarisha mifumo ya usimamizi wa masuala ya msingi, yakiwemo ya usalama na afya mahali pa kazi.

Aliipongeza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kufikia idadi kubwa ya maeneo ya kazi nchini na kuhakikisha wadau wanakua kuhusu usalama na afya kazini.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji majukumu ya ofisi hiyo, Waziri wa Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Waziri Ridhiwani Kikwete, aliishukuru kamati hiyo kuishauri serikali kuhakikisha mipango yake ya maendeleo inafanikiwa.

Akitolea ufafanuzi wa baadhi ya hoja za wajumbe wa kamati hiyo, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kupitia uwezeshaji wa serikali, wamejipanga kujiimarisha zaidi kiutendaji kwa kuongeza vitendea kazi, kujenga miundombinu bora ya kutolea huduma na kuongeza uelewa wa wadau kuhusu masuala ya usalama na afya kazini.

# BAKWATA wajitosa kuimairisha ndoa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoani Singida limeweka mkakati wa kuanza kutoa elimu ya maisha ya ndoa kwa wananchi ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika jamii, talaka na watoto wa mitaani.

Sheikh wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro alitangaza mpango huo jana baada ya viongozi wa BAKWATA kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa huo,Halima Dendego kuhusu azma yao ya kutoa elimu hiyo kwa wananchi.

Sheikh Nassoro, alisema ni wakati sahihi kuhakikisha elimu inatolewa kwa jamii na kuondoa tabia mpya zisizofaa na kuonekana za kawaida katika jamii kwa kuzikomesha ili kukwepa madhara ikiwemo kutalakiana kwa wazazi.

Alisema kutalakiana limekuwa ni jambo linalopunguza upendo na amani kwa watoto wao huku wengi wakikosa mahitaji muhimu kama elimu na uangalizi wa karibu wa malezi bora.

Kwa upande wake Dendego, aliwaahidi viongozi hao kutoa ushirikiano wa kutosha kwa viongozi wa dini kwa kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wanajamii wote .

Alisema ili kufanikisha mpango huo, viongozi na wazazi washirikiane kwa ukaribu kuhakikisha vijana wanarudi katika mienendo bora, kuishi kiimani na kuwa mfano wa kuigwa sio kwa wenzao pekee bali jamii na Taifa.

Dendego, aliwaasa wanajamii kuepuka kutengeneza makundi ya chuki baina ya wazazi kwasababu ya talaka huleta madhara mabaya kwa wote wanaowazunguka hususani watoto kwa kukosa malezi bora na kuishia mienendo isiyofaa.

"Familia ndio jamii, ukishakuwa na familia bora utazalisha jamii bora," alisema Dendego.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekua na ongezeko la ndoa nyingi kuvunjika kwa sababu mbalimbali huku ikidaiwa kuchochewa na mporomoko wa maadili inayochangiwa na malezi yasiyofaa na matumizi mabaya ya teknolojia yanayoendelea kutokea duniani.



## NYANDA ZA JUU KUSINI

# DED aagiza wanafunzi awali wajue kusoma, kuandika, kuhesabu

**Na Mwandishi Wetu,**
CHUNYA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Tamim Kambona amewaagiza walimu wakuu na wa madarasa ya awali kuhakikisha wanafunzi wote wa awali wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu wilayani hapa.

Kambona alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku saba kwa walimu hao kuhusu njia na vifaa vya mtaala wa elimu ya awali vilivyoboreshwa kwa walimu wa shule 48 za halmashauri hiyo.

Alisema hayupo tayari kusikia kuna mwanafunzi hajui kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kuwa katika shule zote wanapata lishe ya kutosha wakati wa masomo na kuwaongezea umakini na uwezo wa kuwasikiliza walimu wawapo darasani.

Kambona, alisema serikali inatumia gharama nyingi kutoa elimu bure, kuboresha miundombinu ya shule na vifaa vya kufundishia, hivyo haoni sababu ya wanafunzi hao kushindwa kusoma, kuandika na kuhesabu.

**"Mwaka huu sitaki kusikia jambo hilo linajitokeza kwenye shule yeyote ile ilihali walimu mko pale na mashahara mnalipwa, hakikisheni kila mwanafunzi anatoka darasa la awali ...**

"Mwaka huu sitaki kusikia jambo hilo linajitokeza kwenye shule yeyote ile ilihali walimu mko pale na mashahara mnalipwa, hakikisheni kila mwanafunzi anatoka darasa la awali akiwa anajua kusoma, kuandika na kuhesabu," alisisitiza.

Aliwataka walimu hao mafunzo waliyopata yakawe msaada mkubwa kwa wanafunzi.

Awali Mratibu wa Miradi ya Boost wa wilaya hiyo, Abdallah Mchelu, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu juu ya miongozo ya elimu ya awali, ushirikishwaji jamii, upimaji katika elimu ya awali na kutengeneza zana zinazotumika kufundishia.

Akizungumza kwa niaba ya walimu walioshiriki mafunzo hayo, Mwalimu wa Shule ya Msingi Nkwangu, Jackson Laizer alisema yatawasaidia kuandaa zana bora na mbinu za ufundishaji kwa wanafunzi kwa ufanisi zaidi.



Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (kushoto), akijadiliana jambo na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Dk. Rashid Chuachua walipotembelea kukagua upanuzi wa uwanja cha ndege wa Kigoma na ujenzi wa jengo la abiria, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango kutokomeza udumavu watoto

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MKOA wa Njombe unatarajia kuzindua mpango harakishi kukabiliana na udumavu watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika maeneo yake.

Mkakati huyo ulielezwa juzi na Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Juma Mfanga wakati wa kikao cha maandalizi uzinduzi wa mpango huo kilichohusisha wawakilishi wa Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF).

Dk. Mfanga, alisema wanatarajia kuzindua mpango huo huo ili kutokomeza udumavu mkoani hapa kwa kusababisha changamoto katika ukuaji wa watoto, maendeleo ya elimu na afya.

Alisema mpango huo utajumuisha afua mbalimbali ikiwemo utoaji elimu kwa wazazi kuhusu lishe bora kwa watoto wachanga na wajawazito, upatikanaji chakula chenye virutubishi kwa kaya zenye watoto walio hatarini na kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto.

Alisema mkoa huo umejipanga kupunguza kiwango cha udumavu kwa watoto ili waweze kuwa katika mazingira yenye lishe bora kwa mustakabali wao na wa taifa.

Mwakilishi wa UNICEF nchini, Ruth Nkurlu, alisema dhamira yao katika kusaidia mpango huo ni kutoa msaada wa kiufundi na rasilimali kuhakikisha watoto wanapata lishe bora na huduma muhimu za afya kwa maendeleo yao.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya, Demografia na Viashiria vya Malaria mwaka 2022, Njombe una kiwango kikubwa cha udumavu kwa asilimia 50.4 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

# Watakiwa kuwa mabalozi wa kilimo

**Na Mwandishi Wetu,**
WANGING'OMBE

VIJANA wametakiwa kuwa mabalozi wazuri wa mabadiliko katika sekta ya kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuweza kuzalisha kwa tija na kukuza uchumi wao.

Wito huo ulitolewa juzi na Mratibu wa Mradi wa YEFFA (Mechanization) chini ya AGRA, Fredi Kamande wakati wa mafunzo kwa vijana 61 kutoka wilaya za Njombe na Wanging'ombe yaliyofanyika Kata ya Ilembula wilayani hapa.

Kamande, alisema vijana hao wamepata mafunzo maalumu ya usimamizi wa zana za kilimo na ubunifu wa teknolojia za kilimo.

"Mafunzo haya yalilenga kuboresha sekta ya kilimo kwa kuongeza tija na ufanisi kupitia matumizi ya teknolojia za kisasa kwa vijana ili waweze kuingia kwenye kilimo wakiwa na ufahamu wa kutosha," alisema.

Alisema hatua hiyo pia inalenga kuwawezesha kujiajiri na kupunguza changamoto za upatikanaji wa teknolojia za kilimo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Lengo letu ni kuwawezesha vijana hawa kuwa mabalozi wa mabadiliko katika sekta ya kilimo kupitia matumizi ya teknolojia za kisasa," alisema Kamande.

Alisema YEFFA unasimamiwa na AGRA kwa ufadhili wa Mastercard Foundation ili kuinua kilimo kupitia teknolojia bunifu.

"Pia unawapatia vijana nafasi ya kuendeleza ujuzi wao na kujipatia ajira endelevu na hii inaendana na malengo ya serikali ya Tanzania ya kukuza sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030," alisema.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliwataka wakulima mkoani humo kutumia teknolojia za kisasa kuongeza tija na ubora wa mazao yao.

"Matumizi ya zana za kisasa za kilimo ni msingi wa mapinduzi ya kilimo. Wakulima wa Njombe wanapaswa kutumia teknolojia hizi ili kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi wa mkoa wetu," alisema.

Alisema Njombe unalenga kufikia malengo ya kitaifa ya kuboresha sekta ya kilimo na kuhakikisha vijana wanapata ujuzi na ajira katika teknolojia za kisasa za kilimo.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Franco Musha, alisema vijana wengi wanaogopa kuingia kwenye kilimo kutokana na zana duni, hivyo kuwepo wa zana za kisasa utakuwa chachu kwa wengi kuingia kwenye sekta hiyo.



# Zanzibar kuongeza uzalishaji mpunga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema mradi wa ujenzi wa mfumo wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde sita kisiwani Unguja na Pemba utaongeza uzalishaji wa mchele na kupunguza kuagiza nje ya nchi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis wakati akizungumza na wakulima wa mpunga baada ya kukagua miundombinu hiyo kwenda katika mashamba yao ya mpunga.

Khamis, alisema miongoni mwa vipaumbele vyake vikubwa serikali ni uzalishaji wa mazao ya chakula ya kutosha ikiwemo mpunga.

Alisema kwa mwaka serikali inaagiza zaidi ya tani 45,000 za mchele kutokana na uzalishaji mdogo wa mpunga visiwani hapa.

Alisema hatua hiyo imeilazimu serikali kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu hiyo kwenda katika mabonde hayo yenye mashamba ya mpunga ya ukubwa wa hekta 1,053. Khamis, aliyataja mabonde hayo kuwa ni Kilombero, Kibokwa, Kinyasini, Chaani na Mlelema kwa upande wa Pemba ambayo ujenzi wa miundombinu yake umekamilika.

**Aliwataka wakulima wa mpunga kuitunza miundombinu hiyo ili kuwawezesha kulima chakula kwa wingi na kuongeza kipato chao.**

Aliwataka wakulima wa mpunga kuitunza miundombinu hiyo ili kuwawezesha kulima chakula kwa wingi na kuongeza kipato chao.

Alisema mradi huo utawanufaisha zaidi ya wakulima 2,100 kwa kuongeza uzalishaji wa mpunga hadi kufikia tani 15 kwa hekta na kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua. "Hii miundombinu imeigharimu serikali fedha nyingi, mnatakiwa kuitunza idumu kwa muda mrefu," alisema Khamis.

Kuhusu pembejeo, alisema serikali imetenga sh.bilioni 5.5 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kupata kwa bei nafuu.

Sekta ya kilimo Zanzibar imeajiri takriban asilimia 35 ya wananchi wa Zanzibar huku asilimia 70 ya wananchi wake wanategemea sekta hiyo kwa ajili ya kujikimu kimaisha.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Migombani, wakiwa kando ya barabara , wakati wa mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume juzi, akitokea jijini Dodoma katika Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM, ambapo aliteuliwa kuwa mgombea Urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wakumbushwa kuhamasisha watoto kupenda kujisomea

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwajengea watoto mazingira mazuri ya kuwahamisisha kupenda kusoma vitabu na kujifunza mambo yenye tija katika maisha yao ya baadae.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar, Safia Ali Rijal kwenye uzinduzi wa kitabu cha wosia kiitwacho 'Soma mwanangu' kinachosimuliwa kwa njia ya sauti uliofanyika Maktaba Kuu Maisara,

Rijal, alisema wazazi na walezi wanatakiwa kuwasimamia watoto wao ili wapende kusoma vitabu vyenye manufaa vinavyoelekeza njia bora za kuishi na jamii inayowazunguka na kujitambua.

Alimpongeza mtunzi wake kwa ubunifu aliotumia kufikisha ujumbe wake kwa njia nyepesi ya sauti, maudhui mwanana na uwasilishaji wake wenye ushairi.

Alisema dunia ya sasa watu wamekuwa na harakati na mbio nyingi za kimaisha, hawapati muda wa kutosha kupumzika na kusoma vitabu vilivyochapishwa.

Alisema mtu anaweza kusikiliza kitabu ambacho maelezo yake yamerikodiwa kwa sauti huku akifanya shughuli nyingine na kufahamu ujumbe uliomo.

"Wazazi wanajitahidi kutoa mafunzo kwa watoto wao, lakini katika dunia ya sasa yenye shughuli nyingi, hawapati muda wa kutosha kuwaambia kila kitu, ubunifu kama huu ni mzuri kwani kitabu kimekusanya mambo mengi yanayowafaa watoto na jamii kwa jumla," alisema Rijal.

Aliwashauri wazazi na walezi wasipuuze jukumu ya malezi ya watoto kwa kisingizio cha hali ngumu ya maisha na kukumbuka nao walilelewa, kutunzwa na kusomeshwa katika hali ngumu zaidi hadi walipofikia.

Aliwataka waandishi wa vitabu, mashairi na maigizo kutumia fani zao kuandaa mbinu za kuwaepusha watoto na vitendo vya udhalilishaji vinavyoendelea kukithiri nchini. Mkurugenzi wa Bodi ya Huduma za Maktaba, Ulfat Abdulaziz Ibrahim, alisema kitabu hicho kinaakisi umuhimu wa teknolojia ya kisasa katika kujifunza na kuwashauri watoto kuitumia vizuri kupata manufaa badala ya kutafuta mambo yasiyofaa kinyume na maadili ya Zanzibar na mafunzo ya dini.

Rijal, alisema yaliyomo kwenye kitabu hicho ni msaada kwa kila mtu katika nafasi yake na kuwashauri wakisikilize, kupitia kundi lao la maktaba kuu.

"Kizazi cha sasa si kama kilichopita, wazazi wetu walipata muda wa kutulia na kusoma vitabu. Dunia ya sasa inatumia zaidi maktaba na inakwenda kidijitali. Itumieni msome ili mpate maarifa na busara vitabuni," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya NOVAVIS International Ltd iliyodhamini uzinduzi wa kitabu hicho, Salma Salim Adim, alisema wasia umekuja wakati mwafaka ambao watoto nchini wanapitia kipindi kigumu cha mmomony'oko wa maadili na kuathiri ustawi wa familia na taifa.

Mtunzi wa kitabu hicho, Nurdin Zuberi Mihungo, alisema anakitoa sadaka kwa kila mtu na anatarajia kukiweka kwenye mtandao na kukichapisha baadae.

Alisema kitakapochapishwa hakitauzwa, ikibidi kufanya hivyo, asilimia 50 ya mapato yatasaidia watoto wenye mahitaji na nyingine, kuchapisha nakala zaidi kwa ajili ya kutoa sadaka.

# Wavuvi wadogo watakiwa kuungana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI wadogo wametakiwa kushirikiana kutumia fursa zilizopo baharini kwa maendeleo yao na taifa.

Mwenyekiti wa Muungano wa Vyama vya Ushirika Zanzibar (CUZA), Suleiman Ame Mbarouk, alitoa wito huo wakati akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Wavuvi Wadogo Zanzibar (ZASFICU), uliofanyika Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja.

Mbarouk, alisema uzoefu unaonesha kuwa bahari inazalisha ajira nyingi hasa kwa vijana na kuwataka kuungana kutumia fursa hiyo kujikwamua kiuchumi.

"Endapo mtashirikiana mtaisaidia Serikali kuendelea kutekeleza azma yake ya kuboresha maisha ya wavuvi kama sera ya uchumi wa buluu inavyoelekeza," alisema.

Mwenyekiti wa ZASFICU, Omar Mohammed Ali, alisema chama hicho kitaendelea kupaza sauti za wavuvi wadogo nchini ili kuhakikisha wanapata tija kupitia shughuli hizo.

"Lengo la chama hiki ni kujikusanya na kuwa na sauti moja katika kusimamia utetezi wa sera na sheria kwa wavuvi zitakazoimarisha maisha yetu," alisema.

Alisema hadi sasa chama hicho kina wanachama kutoka vikundi 57 vya wavuvi huku vingine vikiendelea na taratibu za kujiunga ili kuongeza nguvu kuleta mageuzi chanya ya maisha ya wavuvi.

Ofisa Uvuvu wa Wilaya ndogo Tumbatu, Amour Sheha Khamis, aliwataka wavuvi kuanzisha vikundi rasmi ili kupata mikopo haraka na kuendesha shughuli zao kwa ufanisi na kuboresha maisha yao.

# Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

Na Sabato Kasika



MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Arusha, jijini Arusha, Dayna Paschal (13), ametoweka nyumbani kwao na kwenda kusikojulikana.

Babu wa mwanafunzi huyo, Julius Patrick alisema jana kuwa mjukuu wake alitoweka Januari 20 mwaka huu saa mbili usiku. Wamefungua jalada la tukio hilo katika kituo cha polisi. Namba ya jalada: SOB/RB/80/2025.

"Siku ya tukio, alirudi nyumbani jioni, akaandika ujumbe katika karatasi na kuuacha mezani, ukielezea kuwa amekwenda kwa rafiki yake hadi saa mbili usiku, akawa amerudi nyumbani," alisema Patrick.

Alifafanua kuwa aliporudi, mama yake alitaka waondoke naye hadi kwa rafiki yake athibitishe kama alikuwa huko. Walipotoka tu ndani ili kwenda kwa huyo rafiki yake, alimkimbia mama yake na kwenda kusikojulikana.

"Kwa hiyo tangu wakati huo hatujui aliko, tumemtafuta kwa ndugu, jamaa na marafiki, hayupo! Hivyo tumekuja huku kwenu mtusaidie kututangazia ili kama mtu atamwona, basi atoe taarifa kituo cha polisi au awasiliane na mimi kwa namba 0788-231172," alisema.

# Simbachawene ashtukia mchezo mchafu kwa maofisa utumishi

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amewaagiza makatibu tawala wa mikoa nchini kuwasimamia maofisa utumishi kwenye taasisi za serikali ili kukomesha tabia ya kuwaweka benchi watumishi wanapoajiriwa na kupelekwa mikoani kwa kutowapangia majukumu.

Alitoa agizo hilo juzi mjini hapa baada ya kubaini tabia hiyo miongoni mwa maofisa hao nchini alipopewa taarifa kuhusu hali ya utumishi wa umma kwa mkoa wa Singida wakati akiwa katika ziara yake ya siku moja.

Simbachawe alisema ofisa utumishi ambaye hataki kumpa majukumu mfanyakazi anayeajiriwa, anaipa hasara serikali kwa sababu mfanyakazi huyo analipwa mshahara bila kufanya kazi na ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi, ikiwamo sheria iliyoanzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

"Wapo watu wanakataa kuwapa majukumu na kuhoji 'amekujakujaje hapa? ameletwa na nani?' Ni kwa sababu tu kuna viposho, hivyo wanasema 'huyu atakuwa amekuja kuingilia viposho vyetu'," Simbachawene alisema.

Waziri huyo alisisitiza kuwa maofisa hao ni lazima watambue kuwa kazi ya serikali ni kumpangia mtumishi yeyote inayemwajiri majukumu kuanzia muda anaopangwa kazini asubuhi hadi anapokwisha, vinginevyo ni hasara kwa serikali kwa kuwa analipwa mshahara.

Alisema baadhi ya maofisa hao wanafikiri masuala ya kiutumishi ni jukumu la Waziri wa Utumishi, Katibu Mkuu Utumishi na Sekretarieti ya Ajira. Ni jukumu la wote na likisimamiwa vizuri mambo yatakwenda vyema.

"RC (Mkuu wa Mkoa) kuna jambo lipo, unaletewa mtumishi, lakini mwajiri hataki kumpa majukumu. Utafiti unaonesha kuna watu wanakuwa mahali pa kazi, lakini hawapewi majukumu na mtumishi anakaa miezi minne, mitano anaondoka," alisema.

Vilevile, aliwaagiza wakuu wa mikoa katika vikao vyao vya kujadili maendeleo katika mikoa yao, wazingatie pia masuala ya kiutumishi badala ya kuyaacha kwa maofisa hao kwa kuwa baadhi wanaumiza watumishi.

"Kuna watu wanaoneana sana huko chini, lakini pia wapo watumishi wazembe sana ambao wanatakiwa hata wasiwapo katika utumishi wa umma, lakini wanaachwa," alisema waziri huyo.

Awali Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga alisema halmashauri nane zilizomo mkoani mwake, zina watumishi 11,690 kati ya 20,653 wanaohitajika, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 8,693.

Dk. Fatuma alisema watumishi 4,497 kati 4,701 wenye sifa za kupandishwa vyeo wamepandishwa. Watumishi 204 waliobakia, taratibu zinaendelea ili wapandishwe vyeo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alimhakikishia Waziri Simbachawene kuwa maelekezo yote aliyotoa yatasimamiwa ipasavyo mkoani mwake.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YOHANA DEUS NYABIRI,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya toyota **RAVA 4J** yenye namba za usajili **T 903 ASZ, CHASSIS NAMBA ACA210114692, ENGINE NAMBA 1AZ451909** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/3113/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH OF TANZANIA UNION** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 446 BHD** aina ya **TOYOTA NOAH**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/9215/2025.**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1586 OF 2025**

**In Matter of the Estate of the Late HERMINA AZA FOYA**

**By 1. CHAWESA LENGESELA KAPUNGU**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **24** day of **JANUARY, 2025**
Dated at **Morogoro**, this **22** day of **01, 2025**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SARAH EZEKIEL MEGIROO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 659 DTR - MAZDA AXELA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/10514/2025.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1619 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MELANIA CLETUS AMNAAY**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ROSE JAMALY NGELANGELA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of February, 2025.
Dated at KOROGWE this 22 day of January, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE
PRINCIPLE RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT COURT

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA......106.........MWAKA ........2024**
**PETER WAMBURA......... (MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU RHODA) ..........MJIBU MAOMBI**
**DHIDI YA**
**SIMON ELENESTI............MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA......SAMSON SAMZEGE......**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 29...Mwezi 01......2025 ...Saa 08:30 Asubuhi mbele ya mheshimiwa M. MWINYI ...Mwenyekiti wa Braza, hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wanhu Lakiri/Muhuriwa Braza hili leo tarehe 09....Mwezi ...01...Mwaka.......2025.

**MWENYEKITI.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT OF KASULU**
**AT KASULU**
**CIVIL CASE NO 29920 OF 2024**

**MALAGARASI ENTERPRISE AND CO PLAINTIFF(S)**
**VERSUS**
**SINANI BUILDING CONTRACTORS L DEFENDANT (S)**

**SUMMON TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V, r l Civil Procedure Code)**

**To ...SINANI BUILDING CONTRACTORS L DEFENDANT LIMITED OF DAR ES SALAAM**
**WHEREAS** the above named Plaintiff (s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of plaint;
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that if you default in filing of the written of the statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgement against you.
TAKE FURTHER NOTICE that the case also has been fixed for order before Hon I.E. SHULI-SRM Judge/Magistrate on the 27th day of Jan, 2025 at 8:00 O'clock in the forenoon/afternoon.
GIVEN UNDER MYA HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 13th day of Jan 2025
REGISTRAR/MAGISTRATE
I HEREBY acknowledge the receipt of a duplicate of this summons this ............ day.... of...20...

**DEFENDANT**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI, PIKIPIKI NA BAJAJI

**ABDILAH KHAMIS ALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 471 AUK – NISSAN CIVILIAN.** Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 815 ADH – TVS STAR** na Kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 227 DAT – BAJAJI BOXER.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/15808/2025.**

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI**
**HATI NAMBARI: DSMT1033086**
**MMILIKI: ALLY SALEH POSSI AS GUARDIAN OF AMAL ALLY POSSI, P.O. Box 75218 DSM, DAR ES SALAAM, SHARE (1/1)**
**ARDHI: KIWANJA NA. P25833 KITALU NA. BOKO DOVYA, KINONDONI**
**MUOMBAJI: ALLY SALEH POSSI, WA SLP 75218, KINONDONI, DAR ES SALAAM.**
**AMAL ALLY POSSI, WA S.L.P 75218, KINONDONI, DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA IMETOLEWA** kwamba Hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

**HATI YA ASILI ikionekana, irudishwe kwa**
**Msajili wa Hati,**
**S.L.P 1191**
**DAR ES SALAAM.**


**FORM 58**
**IN THE COURT DISTRICT DELEGATE OF TEMEKE DISTRICT**
**AT TEMEKE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 32002/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANGELINA MICHAEL MSEMWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY FAUSTIN ERASTO KAVISHE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 day of 3....2025.
**Dated at DAR ES SALAAM this 21 day of 1....2025.**

Senior Resident Magistrate

## KUPOTEA KWA CHETI



**IYADY BAIYA MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye namba **PS.2005036/012** kilichotolewa na **SHULE YA MSINGI KIPUMBWI PWANI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PAN/B.1/19/VOL.1.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 31289/2024**
**In the matter of the Estate of the late FRANK RICHARD MGAYA of Line Polisi Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOHN ELIYA MGAYA NA JANETH KENETH KISEBO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23 Day of 1, 2025

..................................
**1ST PETITIONER**

..............................
**2ND PETITIONER**
**Presented for filling this 12 day of 12,2024**

.................................
**RESIDENT MAGISTRATE**



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Feza Boys, wakishangilia huku wakiwa wamembeba juu mwanafunzi mwenzao, Alan Masaka, shuleni hapo, Dar es Salaam jana, aliyefanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne kwa kupata ufaulu wa alama divisheni A.7 . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hisabati bado shubiri kidato cha nne

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2024, yakionesha ufaulu kwenye somo la hisabati bado uko chini.

Matokeo hayo yanaonesha kuwa watahiniwa wa shule 477,262 ambao ni miongoni mwa watahiniwa 516,695 wenye matokeo, wamefaulu sawa na asilimia 92.37, wakipata madaraja I, II, III na IV.

Mwaka 2023 watahiniwa waliofaulu walikuwa 471,427 sawa na asilimia 89.36, hivyo ufaulu umeongezeka kwa asilimia 3.01.

Kati ya watahiwa 477,262 waliofaulu, wasichana ni 249,078, sawa na asilimia 91.72 ya wasichana wote wenye matokeo na wavulana ni 228,184 sawa na asilimia 93.08 ya wavulana wenye matokeo.

Akitangaza matokeo hayo jana, jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Mohamed, alisema somo la Hisabati (Basic Mathematics) lina ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni asilimia 25.35.

Dk. Mohamed alisema takwimu za miaka 10 za somo hilo zinaonesha mwaka 2015 ufaulu ulikuwa wa asilimia 16.76 na mwaka 2024 ni asilimia 25.35, hivyo juhudi za ziada zinahitajika ili kuinua ufaulu.

„Ufaulu wa somo la Basic Mathematics umeshuka kidogo kwa asilimia 0.07 na katika somo la Additional Mathematics umeshuka kwa asilimia 2.70 kulinganishwa na ufaulu wa mwaka 2023. Ubora wa ufaulu umeshuka kidogo katika somo la Basic Mathematics kwa asilimia 1.04,“ alifafanu.

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa masomo ya kemia, kilimo, Engineering Science, Information and Computer Studies, Additional Mathematics na Food and Human Nutrition ni kati ya asilimia 93 na asilimia 100.

Alisema ufaulu wa juu uko katika somo la food and human nutrition ambalo watahiniwa wote waliofanya somo hilo walifaulu likifuatiwa na somo la kemia asilimia 96.36.

Alisema masomo yote ya sayansi jamii yameongezeka ufaulu kati ya asilimia 2.51 hadi 10.16 kulinganishwa na ufaulu wa mwaka 2023.

Dk. Mohamed alisema jumla ya watahiniwa 15,185 wa shule na wa kujitegemea waliosajiliwa kufanya mtihani, hawakufanya mtihani huo. Kati yao, wa shule ni 11,869, sawa na asilimia 2.24 na wa kujitegemea ni 3,316 sawa na asilimia 11.65.

Alisema kuwa kati ya watahiniwa 529,329 wa shule waliosajiliwa, watahiniwa 517,460 sawa na asilimia 97.76 walifanya mtihani huo, Kati yao, wasichana ni 271,918 sawa na asilimia 97.54 ya wasichana wote.

Alisema wavulana ni 245,542 sawa na asilimia 98 ya wavulana wote na kati ya watahiniwa 28,467 wa kujitegemea waliosajiliwa, 25,151 sawa na asilimia 88.35 walifanya mtihani huo.

Katibu Mtendaji alisema baraza limefuta matokeo yote ya watahiniwa 67 waliobainika kufanya udanganyifu na watahiniwa watano walioandika lugha ya matusi katika karatasi zao za majibu.

Dk. Mohamed alisema matusi hayakubaliki mahali popote na kusisitiza watahiniwa kuzingatia maadili na jamii kuendelea kukemea jambo hilo.

Alisisitiza kwamba tayari wameshaziandikia barua shule walikokuwa wanasoma wanafunzi walioandika matusi ili kutoa taarifa kwa wazazi wao, wawachukulie hatua za kimaadili.

„Baraza limefungia kituo cha P6384 BSL Open School kilichoko mkoa wa Shinyanga kuwa kituo cha mitihani ya taifa kutokana na kuratibu mipango ya udanganyifu na shauri liko mahakamani,“ alisema.

Dk. Mohamed pia alisema baraza limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 459 ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani huo. Watarudia kufanya mtihani mwaka huu.

# TMA yatoa hadhari athari kiuchumi mvua ya masika

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imewataka wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za mamlaka hiyo ili kuepuka maafa.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alitoa rai hiyo jana Dar es Salaam alipotoa mwelekeo wa mvua ya msimu wa masika kuanzia Machi hadi Mei, mwaka huu.

Katika sekta ya kilimo na usalama wa chakula, alisema vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua ya wastani.

Alisema wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea yanayoendana na hali ya ongezeko la unyevu, kama vile ukungu, yanatarajiwa kuongezeka na kuathiri mazao kama ndizi, mahindi, mpunga, mihogo na maharage.

"Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa kuzingatia hali ya unyevu katika udongo, kutumia mbinu bora za teknolojia kuzuaia maji kutuama shambani. Sambamba na hilo, wanatakiwa kuzuia mmomonyoko na upotevu wa rutuba kutokana na kutwamisha maji kwa muda mrefu au mafuriko," alisema.

Dk. Chang'a alisisitiza kuwa wakulima wanashauriwa kufuata taarifa sahihi kutoka kwa maofisa ugani kwa kuzingatia utabiri wa msimu wa wilaya husika katika kuchagua mbegu sahihi.

Katika sekta za mifugo na uvuvi, alisema kunaweza kutokea mlipuko wa magonjwa ya mifugo kama vile homa ya bonde la ufa, miguu na midomo na kuzaliana kwa wadudu waharibifu.

Alisema pia upungufu wa maji unaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho hivyo wafugaji wanashauriwa kutumia taarifa za TMA, na kuzingatia taarifa zinazotolewa na maofisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Katika sekta za utalii na wanyamapori, alisema mvua chini ya wastani inayofanya maji kutuama na kusambaa, inaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa kati ya wanyamapori na wanaofugwa.

Alisema kutokana na hali hiyo, TMA inashauri mamlaka husika kuboresha miundombinu mbalimbali katika mbuga na mapori ya akiba na kujenga uelewa wa jamii ili kuchukua hatua stahiki kuhusu athari zinazoweza kujitokeza.

Katika sekta ya usafiri na usafirishaji, alisema katika maeneo yanayoweza kupata mvua ya wastani wa chini na wa juu unaweza kujitokeza uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli sambamba na kuongezeka kwa ajali za usafiri wa nchi kavu.

Pia alisema kunaweza kujitokeza matukio ya kuchelewa au kuahirishwa kwa safari za anga na majini pamoja na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji.

"Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kutekeleza ujenzi wa miundombinu pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara," alisema Dk. Chang'a.

Katika sekta za nishati na madini, alisema kutakuwapo na ongezeko la vina vya maji linalotarajiwa kujitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua ya wastani hadi juu yake, hivyo kusababisha mafuriko.

Alizitaka mamlaka husika kuchukua hatua stahiki ili kuepuka athari za miundombinu hiyo ili kunusuru sekta hiyo. Pia alizishauri mamlaka za miji na wilaya kutoa elimu ya uelewa kwa timu mbalimbali za usiamamizi kuhusu hali ya hewa inayotarajiwa katika msimu huu.

Katika sekta ya afya, alisema uharibifu wa miundombinu ya maji unaweza kusababisha maji ya mvua kutuama na kutiririka katika makazi ya watu, hivyo kusababisha uchafuzi wa maji na magonjwa ya mlipuko. Alizishauri mamlaka za afya kupunguza athari hasi za kiafya kwa kuharibu mazalia ya mbu, na kutibu maji kabla ya kuyatumia.

Kuhusu sekta binafsi, alisema shughuli za kilimo na uzalishaji viwandani zinaweza kuathirika kutokana na upungufu wa malighafi za kilimo unaotokana na upungufu wa mvua hususani kwenye maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini yake.

Alisema hali hiyo, inaweza kusababisha ongezeko la gharama za upatikanaji malighafi na uendeshaji. Upungufu wa mvua unaweza kuathiri ubora wa bidhaa.

"Wadau wa sekta hii wanashauriwa kushirikiana na wataalamu na taassi mbalimbali ikiwamo TMA ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza, taasisi za benki na bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara" alisema Dk Chang'a

Vilevile alivitaka vyombo vya habari kutoa taarifa kwa wakati ili kuelimisha umma kuhusu athari zinazoweza kujitokeza huku akisisitiza mamlaka hiyo itaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho.

# AZAM YAIMARISHA MIPANGO LALA SALAMA IKIITAJA KMC FC

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Azam FC umesema utaanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu timu nyingi zimeboresha viwango vya vikosi vyake tofauti na ilivyokuwa katika hatua ya awali, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana kuelekea mzunguko wa pili, Ofisa Habari wa Azam, Hasheem Ibwe, alisema watacheza mechi kwa umakini na wamejiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa timu pinzani.

Ibwe alisema baada ya kubaini mapungufu katika mzunguko wa kwanza, timu zimefanya usajili wa kuongeza wachezaji bora na hii itaongeza ugumu katika kila mechi watakayocheza.

"Sisi tunajiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara, malengo yetu ni kufanya vizuri kwenye ligi na Kombe la FA, tunafanya maandalizi mazuri na mbinu za mwalimu wetu (Rachid Taoussi), naamini zitatusaidia.

Mzunguko wa pili naamini utakuwa mgumu zaidi, kwa sababu timu nyingine zina walimu wengi wazuri, zimejiimarisha zaidi, nyingi zilileta ushindani mkubwa mzunguko wa kwanza, huu wa pili zimefanya usajili mzuri kuelekea, tuliona hata viwango vya mchezaji mmoja mmoja kwenye timu nyingi ni vizuri sana," alisema Ibwe.

Hata hivyo aliongeza haimaanishi wanaziogopa, badala yake wanataka kuongeza umakini ili kuvuna pointi nyingi ambazo zitawasaidia kufikia malengo.

„Hatuhofii kukutana na yoyote, tunachotaka ni kukusanya pointi nyingi ili zitusaidia huko mbele," Ibwe alisema.

Aliongeza kwa sasa kikosi chao kiko kwenye maandalizi makali kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC, unaotarajiwa kuchezwa Februari 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Thabit Zacharia, alisema watakuwa wakifanya mazoezi kwa siku saba na baada ya hapo watacheza mechi ya kirafiki.

"Kila wiki tutakuwa tunacheza mchezo wa kirafiki ili kocha ajue ni wapi wachezaji wake wamemwelewa na wapi wanatakiwa kurekebishwa," alisema Thabit, maarufu kama Zaka Zakazi.

Azam FC inashika nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 36, baada ya kucheza michezo 16.



Baadhi ya waimbaji wa kwaya ya Gethsemane ya kanisa la SDA Kinondoni jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gethsemane yafyatua kibao kipya

**Na Mwandishi Wetu**

KWAYA ya Gethsemane Group ya Kinondoni (GGK), ambayo iko chini ya Kanisa SDA la jijini, Dar es Salaam imezindua wimbo mpya maalumu kwa ajili ya sherehe za harusi uliopewa jina la ‚Ni Siku Yetu'.

Wimbo huo umezinduliwa jijini, juzi na tayarì umeanza kusikika katika vituo mbalimbali vya redio pamoja na mitandao ya kijamii.

Akizungumza kuhusu uzinduzi wa wimbo huo, Mwenyekiti wa kwaya hiyo, Samora Sadick, alisema lengo la kibao hicho ni kuwabariki maharusi na kumtukuza Mungu katika siku ya harusi yao.

Samora alisema wimbo huo umerekodiwa katika Studio ya Katumbo Music ya jijini huku video yake ikiwa imeadakuwa na mwongozaji mkongwe, Joowzey.

"Mikakati ya kwaya yetu baada ya wimbo huu ni kuzindua album mpya inayotarajiwa kutoka mwaka huu 2025. Kwaya ya Gethsemane inatoa wito kwa waimbaji wengine kuendelea kutoa nyimbo za kumtukuza Mungu na kutoa mafundisho mbalimbali kwa jamii.

Kwaya hii inaendelea kujivunia kuwa kwaya iliyojikita katika huduma zaidi ikiwa imepata nafasi ya kutoa huduma ya uimbaji katika shughuli mbalimbali ikiwamo ndani na nje ya nchi. Mwaka 2024 GGK ilipata mialiko miwili ya kuhudumu katika mikutano mikubwa ya injili ya makambi jijini Nairobi, Kenya," alisema Sadick.

Aliongeza wataendelea kutoa elimu na mafunzo kwa jamii kupitia tungo mbalimbali watakazozitunga.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### WIZARA YA UJENZI
### TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

**TANGAZO LA MAFUNZO YA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LABOUR BASED TECHNOLOGY'**

**1. UTANGULIZI:**

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) ni Taasisi ya Wizara ya Ujenzi yenye makao yake makuu Morogoro. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha mafunzo ya kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo na Changarawe kwa makundi maalum ya wanawake, vijana, wazee na wenye ulemavu katika tawi la Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana, wazee na wenye ulemavu katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe na udongo (Gravel and Earth Road) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 17/03/2025 – 12/04/2025 | **Mkoani Mbeya (ICoT) - Mbeya** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za Udongo na changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kuwawezesha makundi maalum kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**

Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**

Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**

Lugha itakayo tumika katika kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi kwa gharama ya ada kiasi cha Tsh. 700,000.

Ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia **'Control Number'** itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi tajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**

**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz,

## ZISIKUPITE

### RASHFORD ANUKIA BARCA
WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, walikutana na viongozi wa Barcelona siku ya Jumanne huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitafuta njia ya kuondoka Manchester United. ***(Sky Sports)***

### SESKO KUTUA ARSENAL
ARSENAL inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Slovenia na klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 21. ***(Sportsport)***

### WALKER ATAJWA MILAN
AC Milan imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa England, Kyle Walker, mwenye umri wa miaka 34, kutoka Manchester City ambapo atatua kwa mkopo, lakini usajili wake unajumuisha chaguo la kumnunua moja kwa moja kwa euro milioni 5. ***(Sky Sports Italia)***

### GARNACHO AITAKA CHELSEA
WINGA wa Manchester United, Alejandro Garnacho, anapendelea kuhamia Chelsea badala ya Napoli, ambako ombi lao la kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 20 limekataliwa. ***(TyC Sports)***

### ADEYEMI KUTUA NAPOLI
NAPOLI inataka kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 23, kutoka Borussia Dortmund. ***(Fabrizio Romano)***

### WATATU KUIHAMA CHELSEA
WACHEZAJI watatu wa Chelsea huenda wakakihama klabu hiyo mwezi huu huku mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ureno, Renato Veiga, mwenye umri wa miaka 21, akishinikiza kuungana na Juventus ***(Mail)***

### CUNHA ANUKIA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest inaandaa dau la kubwa ambalo huenda likafikia pauni milioni 60, ili kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Matheus Cunha, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Wolves. ***(Sky Sports)***

### LUIZ AGOMBEWA ULAYA
JUVENTUS imeipa Chelsea fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz, mwenye umri wa miaka 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal. ***(TeamTalk)***

### TANO ZAMTAKA POGBA
KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 31, anazingatia ofa kadhaa kutoka kwa timu za ligi tano kuu za Ulaya, lakini makubaliano ya mkataba hayajafikiwa. ***(ESPN)***

### STEIDTEN MAMBO MAGUMU
MUSTAKABALI wa Mkurugenzi wa Ufundi wa West Ham, Tim Steidten, katika klabu hiyo uko mashakani baada ya wagonganyundo hao kukamilisha dili la kumsajili mchambuzi wa masuala ya uajiri wa Chelsea, Kyle Macaulay, ambaye amewahi kufanya kazi na Kocha, Graham Potter. ***(Guardian)***

### EVERTON YAMTAKA EMERSON
WAKALA wa Emerson Royal wa AC Milan mwenye umri wa miaka 26, amezungumza na Everton na Fulham, lakini beki huyo wa Brazil pia analengwa na Galatasaray. ***(Calciomercato)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS AKARIBIA REKODI YA RONALDO REAL MADRID

**Ni baada ya kufikisha mabao 100 akiwa ameitumikia timu hiyo...**

**MADRID, Hispania**

VINICIUS Júnior alisema anaiangalia rekodi ya Ronaldo Nazario ya kuwa Mbrazil aliyeifungia mabao mengi zaidi Real Madrid, baada ya kupachika bao lake la 100 wakati timu hiyo ikipata ushindi wa 5-1 dhidi ya RB Salzburg kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya juzi.

Mabao mawili kutoka kwa Rodrygo, yote kwa asisti ya Jude Bellingham, yaliiweka Madrid 2-0 hadi mapumziko kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, kabla ya Kylian Mbappé kuongeza bao la tatu.

Vinícius alifunga mara mbili kukamilisha ushindi huo, na kuwahakikishia Madrid nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano wa michuano hiyo.

Vinicíus sasa ameifungia Madrid mabao 101 katika michuano yote, na hivyo kuikaribia rekodi ya gwiji wa Brazil Ronaldo, ambaye alifunga mabao 104 katika kipindi cha miaka mitano katika klabu hiyo kati ya mwaka 2002 na 2007.

"Nina furaha kufunga mabao katika jezi hii," alisema Vinicius akiiambia Movistar baada ya mchezo huo.

"Nimebakiza mabao matatu kutoka kwa Ronaldo, kutokana na kuwa Mbrazil mwenye mabao mengi kwenye jezi hii. Tutegemee kuwa naweza kufunga zaidi."

Vinicíus ameshinda Ligi ya Mabingwa mara mbili -- akifunga katika fainali zote mbili -- akiwa na Madrid, pamoja na mataji matatu ya LaLiga.

Na pia alishangaa kujua kwamba alikuwa mchezaji bora wa mchezo huo dhidi ya Salzburg.

"Nilikuwa na hisia kwamba singeweza kucheza vizuri katika kipindi cha kwanza," alisema.

"Rodry alistahili, Jude pia, na wachezaji wengi. Lakini nina furaha na ushindi na mabao, hata nilipocheza vibaya."

# Rice ausifia muundo wa Ligi ya Mabingwa

**LONDON, England**

HISABATI ilikuwa inaumiza vichwa kwa baadhi ya wachezaji baada ya ushindi wa Arsenal wa mabao 3-0 dhidi ya Dinamo Zagreb, lakini Declan Rice aliupa tano muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Imekuwa nzuri sana. Ni mara ya kwanza kuijaribu na nadhani kila mtu alichanganyikiwa kidogo jinsi itakavyofanya kazi mara ya kwanza ilipotangazwa, lakini kucheza katika muundo huu kumekuwa kwa kuvutia sana," alisema kiungo huyo baada ya mchezo huo.

"Kucheza na timu kubwa, kuja dhidi ya wapinzani tofauti, nimeipenda sana."

Rice alifunga bao la kwanza huku Arsenal wakijihakikisha kutinga kwenye nane bora kati ya timu 36 ya hatua ya makundi ambayo msimu huu ilibadilisha muundo.

Wako katika nafasi ya tatu wakiwa na alama 16 na kwa kweli wanaweza kuanza kupanga kwa awamu ya mtoano.

"Hatujaambiwa. Najua tuko katika nafasi nzuri sana," alisema Kocha, Mikel Arteta baada ya Arsenal kuendeleza mbio zao za kutopoteza nyumbani kwenye michuano ya Ulaya hadi mechi 15.

Kai Havertz alifikisha jumla ya mabao 14 kwa msimu kwa kufunga bao la pili la Arsenal naye Martin Ødegaard akafunga goli lake la kwanza tangu Novemba dakika za lala salama na kuhitimisha ushindi huo mnono.

"Kwa ujumla, tulifanya kazi na kuifanya vizuri. Hatukuruhusu shuti lililolenga lango ambalo ni chanya tena. Inaonyesha timu iko vizuri," aliongeza Arteta.

"Kwa ujumla, kufunga mabao matatu, kushinda Ligi ya Mabingwa nyumbani, bao jingine safi nyumbani, manne mfululizo, nimefanya mabadiliko makubwa.

"Tulizungusha wachezaji ambao hawakucheza kwa dakika nyingi na walijibu vyema."

## Barcelona wateta na Rashford



**BARCELONA, Hispania**

WAWAKILISHI wa Marcus Rashford wamefanya mazungumzo ya ana kwa ana na Barcelona kuhusu uwezekano wa usajili wa mchezaji huyo kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho, kwa mujibu wa ESPN.

Rashford anapatikana mwezi huu baada ya kukosa nafasi kwenye Uwanja wa Old Trafford chini ya Kocha Mkuu, Ruben Amorim.

Vyanzo vilisema United wako tayari kusikiliza ofa za mkopo, ingawa watadai klabu yoyote inayovutiwa lazima ilipe angalau sehemu ya mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. Wameomba kufahamishwa kuhusu maendeleo ya mustakabali wake, lakini wana matatizo ya kifedha ya kuyatatua kabla ya kuanza mazungumzo rasmi na United.

Kuna uwezekano Barcelona italazimika kutafuta njia za kuwaondoa Eric García na Ansu Fati ili kujipa uwezo wa kifedha kumnunua Rashford.

Vyanzo viliiambia ESPN kuna mashaka katika klabu ikiwa wanamhitaji Rashford kwa sababu nafasi ya kushoto inachezwa na Raphinha, lakini Rais, Joan Laporta, anaaminika ni shabiki wa mchezaji huyo wa England.

Rashford hajaichezea United tangu iliposhinda 2-1 dhidi ya FC Viktoria Plzen Desemba 12 huku Amorim akimlaumu kuhusu uchezaji wake mazoezini.

Alifanya mazoezi ya kawaida na kikosi cha United huko Carrington Jumatano asubuhi kabla ya mechi ya Ligi ya Europa dhidi ya Rangers jana Alhamisi. Borussia Dortmund pia imekuwa ikihusishwa na Rashford, lakini kuna shaka iwapo timu hiyo ya Bundesliga inaweza kumudu kulipa sehemu kubwa ya mshahara wake wa pauni 300,000 kwa wiki.



## GUARDIOLA: CITY BADO NAFASI YA MWISHO UEFA

**PARIS, Ufaransa**

PEP Guardiola amesema Manchester City wana "nafasi moja ya mwisho" ya kujiokoa katika kampeni yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kichapo cha mabao 4-2 kutoka kwa Paris Saint-Germain na kuwaacha wakikabiliwa na aibu ya kuondolewa mapema kwenye mashindano hayo.

Licha ya kuchukua uongozi wa mapema wa mabao 2-0 katika kipindi cha pili kupitia kwa Jack Grealish na Erling Haaland, City ilijikuta ikipoteza mchezo huo pale Parc des Princes.

Matokeo hayo yanamaanisha City lazima sasa waifunge Club Brugge mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Etihad Jumatano ijayo ili watinge hatua ya mchujo.

Na baada ya mchezo huo Guardiola hakuwa na malalamiko yoyote kuhusu matokeo zaidi ya kusema wana nafasi moja ya mwisho.

"Tuna nafasi ya mwisho dhidi ya Brugge na ikiwa hatutapita ni kwa sababu hatukustahili," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Usiku wa leo (juzi), [PSG] walikuwa bora zaidi. Hongera PSG nakubali. Sheria ya soka iko hivyo, jinsi walivyokuwa wakali katika nafasi muhimu wakaweza kurejea mchezoni na kupata ushindi.

"Wachezaji wao walipambana na walikuwa bora zaidi. Walikuwa bora zaidi kwenye mechi."

City ilisalimisha nafasi ya ushindi kwa mara ya tisa msimu huu na kipigo hicho kilikuwa kupoteza kwao mara ya tatu mfululizo ugenini katika Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kucheza mechi 12 ugenini bila kupoteza katika mashindano hayo.

Naye Guardiola alisema alihisi kipigo hiko kwa City kilitokana na kushindwa kutawala mchezo katika eneo la kiungo dhidi ya kikosi cha PSG.

"Walipokuwa na mpira, walikuwa makini na kututengenezea matatizo," alisema Guardiola.

"Baada ya 2-0 na haswa 1-2 hatukuweza kucheza. Lazima ucheze na mpira na walikuwa bora zaidi."

HABARI MICHEZO

# COPCO, KILIMANJARO SOKONI ZIKIWAKABILI SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Copco FC inayojiandaa kuivaa Yanga katika mechi ya raundi ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam imesema wachezaji wake watatumia mchezo huo kusaka nafasi ya kusajiliwa na vigogo hao.

Kauli hiyo pia imeungwa mkono na mabosi wa Kilimanjaro Wonders ambayo itacheza Jumapili itawakabili Simba katika mashindano hayo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, viongozi wa timu hizo wameonekana kufurahia kucheza na vigogo hao licha ya ugumu ambao wanatarajia kukutana nao katika mechi hizo.

Meneja wa Copco, yenye maskani yake jijini Mwanza, Juma Kisuse, alisema kikosi cha wachezaji 20 na viongozi saba wa timu hiyo kiko kamili Dar es Salaam tayari kwa mchezo huo, huku akisema ni fursa adhimu kucheza na Yanga.

"Yanga ni timu kubwa, ambayo kila mtu anatamani kucheza nayo, tumepata nafasi ya kucheza nayo, hii ni fursa nzuri ya wachezaji wangu kufanya vitu vizuri, kuonyesha uwezo katika mchezo huo ili kupata nafasi ya kujiuza, nimewaambia wapambane ili wapate soko, kama si kwa timu hiyo basi nyingine ambazo zitakuwa zinaangalia mechi hiyo," Kisuse alisema.

Aliongeza ili kujiimarisha kuwakabili mabingwa hao watetezi, kikosi chake kimecheza mchezo mmoja wa kirafiki dhidi ya Pamba Jiji.

"Maandalizi yetu ni mazuri na ndiyo maana tukaamua kujipima na Pamba Jiji kwa sababu timu hiyo na Yanga zote zipo Ligi Kuu," alisema Kisuse, meneja wa timu hiyo inayoshiriki First League zamani Ligi Daraja la Pili.

Naye Mkurugenzi wa Kilimanjaro Wonders, Laurent Kinabo, alisema kwao kucheza dhidi ya Simba ni fursa kubwa ambayo itawafanya wachezaji wake baada ya hapo kujiamini kucheza na timu yoyote ile.

"Hii ni fursa kubwa sana kwetu kucheza na Simba, mechi hii itawatengenezea wachezaji wangu kuanza kujiamini, pia matumaini ya kutimiza ndoto zao kupitia mechi hiyo, wanahitaji kujituma na kuonyesha walichonacho ili kupata soko la usajili msimu ujao," alisema Kinabo, ambaye timu yao inashiriki Ligi ya Mkoa Kilimanjaro.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa (kushoto), akipokea mpira kutoka kwa mwamuzi, Amina Kyando kutoka Morogoro baada ya kufunga hat-trick katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Mlandizi Queens iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 11-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Kombe la Chalenji kufanyika Juni

**Na Somoe Ng'itu**

MASHINDANO ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yamepangwa kufanyika kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, mwaka imefahamika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, aliliambia gazeti hili, kalenda ya mashindano yote ya ukanda huo yalipitishwa katika mkutano mkuu wa baraza hilo uliofanyika mjini Juba nchini, Sudan Kusini jana.

Gecheo alisema mkutano huo pia ulipitisha mashindano ya Kombe la Kagame (Dar Port Kagame Cup 2025), yatafanyika kuanzia Agosti 31 hadi Septemba 14, mwaka huu huku michuano ya soka la ufukweni itachezwa kati ya Mei 31 na Juni 7 nchini Kenya.

Alisema mashindano ya Chalenji kwa wanawake yatatangazwa baadaye huku michuano ya ngazi ya klabu ikipangwa kucheza kati ya Septemba 20 na Oktoba 4, mwaka huu.

"Vyama wanachama wa CECAFA wanatakiwa kutuma maombi ya kuwa wenyeji wa moja ya michuano hii iliyotangazwa ili kuhakikisha kalenda yetu ya mwaka 2025 itatekelezwa vyema," alisema Gecheo.

Red Arrows ya Zambia ndio mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la Kagame iliyofanyika Dar es Salaam mwaka jana wakati kwa wanawake, Simba Queens ya Tanzania Bara ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo.

## Yanga: Tutarejesha furaha yetu kesho

INATOKA UK. 24

naweza kulala vizuri na kuamka vibaya.

Hata wao wamehuzunika, wamenihakikishia hasira zao watazirudisha katika Ligi Kuu wakianza kesho dhidi ya Copco, tunawaomba wanachama na mashabiki wa Yanga waendelee kutuunga mkopo na kuwa nyuma ya wachezaji wetu kila mechi wajitokeze kwa wingi uwanjani," alisema Kamwe.

Wakati huo huo wachezaji wa zamani wa Yanga wamejitokeza kuelezea kilichosababisha timu hiyo kutolewa ni wachezaji kuwa wazito.

Stephano Mwasika, beki wa kushoto wa zamani wa timu hiyo, alisema katika mechi dhidi ya Waarabu, wachezaji wa Yanga walionekana wakicheza tofauti na walivyotegemewa.

"Tulionekana kucheza lakini hatukuonekana kutafuta ushindi tangu dakika ya kwanza, wachezaji walionekana wazito tofauti na watu walivyokuwa wakitegemea, sijui waliamka vipi, lakini timu nzima haikucheza vizuri. Nadhani kwa sasa kila mtu atulie kwa sababu tuna michezo ya Ligi Kuu na Kombe la FA, tunatakiwa kufanya vizuri pia," Mwasika, ambaye aliichezea Yanga kuanzia 2010, hadi 2013 akitokea Moro United alisema.

Aliyekuwa straika hatari wa timu hiyo kati ya mwaka 1990 na mapema mwaka 2000, Mohamed Hussein ,Mmachinga', aliwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kujua kuwa mpira una matokeo matatu hivyo wanatakiwa kutulia baada ya jambo hilo kutokea.

Mmachinga alisema utulivu pekee ndiyo utakaowafanya wachezaji na viongozi wapate nguvu ya kufanya vyema katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na FA na hatimaye kutetea mataji hayo.

"Mpira una matokeo matatu, ukiwa kama mwanamichezo ni lazima upokee matokeo yote, kikubwa ni kujipanga kuangalia tutafanya nini baadaye na kwa sababu tunarudi kwenye ligi, nguvu zetu sasa zote tuhamishie huko tupate ubingwa," alisema Mmachinga ambaye pia aliwahi kuicheza Simba.

Yanga ilianza na mguu mbaya katika mechi za hatua ya makundi baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan na kwenda kufungwa idadi kama hiyo ya magoli ugenini Algeria na wenyeji MC Alger.

Katika mechi ya mwisho, Yanga ikihitaji ushindi wowote ili isonge mbele, MC Alger wao walihitaji sare ya aina yoyote ili kutinga hatua ya robo fainali, na sare ya bila kufungana iliwabeba Waarabu hao.

Baada ya mchezo wa kesho, Yanga itawakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex.


Michezo

Ijumaa Januari 24, 2025

Nipashe

**Guardiola: City bado nafasi ya mwisho Uefa**

UKURASA 22



# Simba, Tabora Utd zatunishiana misuli

## ●●●Mnyama asema ina haki yao kutamba, yaonya isiwafananishe na...

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA ya jijini, Dar es Salaam imewaonya Tabora United haiwezi kuwazuia kupata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Wekundu wa Msimbazi wametamba kamwe Tabora United haitaweza kufanya kile ilichowafanyia Yanga na Azam FC na kuwataka wajiandae ‚kuteseka' katika mchezo huo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana, amezisikia tambo za Tabora United wameangusha vigogo vyote na aliyebaki ni Simba tu, hivyo kuwatahadharisha msimu huu wamedhamiria kupata ushindi kwenye uwanja wowote na kwa timu yoyote wanayokutana nayo.

"Wana haki ya kutamba, wamefanya mambo makubwa, wamechukua pointi tatu dhidi ya Yanga na Azam FC, si jambo dogo, wana haki ya kujivunia, lakini wasitufananishe na watu wengine, kama mzunguko wa kwanza wanasema tuliwakuta hawajakaa vizuri, basi wajue hata Februari 2, tukiwafunga watasema tena hawajakaa vizuri.

Sisi msimu huu tumedhamiria kufanya vyema na tunataka kushinda kila mchezo, tunawaheshimu wana timu ngumu, wana morali ya kutosha, lakini siyo timu ya kutuzuia sisi," Ahmed alisema.

Ahmed alisema kikosi cha Simba kilitarajia kurejea kambini leo baada ya mapumziko waliyopewa kufuatia kumaliza kibarua cha michezo ya hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya CS Constantine na kuongoza Kundi A.

"Tunarejea uwanjani kesho tarehe 24 (leo), kwa sababu tarehe 26 (Jumapili) tuna mchezo dhidi ya Kilimanjaro Wonders, tangu walipocheza dhidi ya CS Constantine vijana walipewa mapumziko, baada ya mchezo huo kambi haitavunjwa, itaendelea kwa ajili ya mchezo wa Februari 2 dhidi ya Tabora United," Ahmed alisema.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, ameendelea kutamba sasa wanamsubiri kumfunga Simba kama walivyotembeza kichapo walipokutana na Yanga na Azam.

Mwagala alisema Simba inatakiwa ijiandae kupita katika njia ambayo ‚wenzake' wamepita msimu huu walipokutana nao.

Tabora United ambayo haikuanza vyema msimu chini ya Kocha Mkenya, Francis Kimanzi, ambaye alitimuliwa lakini iligeuka ghafla na tishio ilipomtwaa Mkongomani, Anicet Kiazmak, aliyebadilisha kwa kiasi kikubwa na kuanza kutoa vichapo vya kushangaza.

Novemba 7, mwaka jana ilitoa kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Yanga mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex huku Desemba 13, ikiwaadhibu Azam FC, mabao 2-1.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Agosti 18, mwaka jana Tabora United ilichapwa mabao 3-0 na Simba, lakini ikidai matokeo hayo yalisababishwa na baadhi ya wachezaji wake wa kigeni kukosa vibali vya kucheza soka hapa nchini.

Hata hivyo, kabla ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba itakutana na Kilimanjaro Wonders katika mchezo wa raundi ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Ligi Kuu Tanzania Bara imerejea tena mapema baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutangaza kusogeza mbele Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambayo awali ilitarajia kufanyika kuanzia Februari Mosi, mwaka huu.

# Yanga: Tutarejesha furaha yetu kesho



Pacome Zoazoua

**Na Adam Fungamwango**

ILI kupoza maumivu ya kutolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa Yanga umesema kikosi chao kimejipanga kutoa vipigo katika kila mechi watakayocheza wakianza na mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Copco FC utakaochezwa kesho, imeelezwa.

Yanga inatarajia kuikaribisha Copco katika mechi ya raundi ya tatu ya michuano ya Kombe la FA itakayochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema si wanachama, mashabiki na viongozi wa timu hiyo pekee ndio waliohuzunika baada ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa, bali hata wachezaji pia waliumia.

Kamwe alisema ili kuendelea upya na safari ya kutetea ubingwa wa FA na Ligi Kuu Tanzania Bara, wachezaji wa Yanga wameahidi kuwafuta machozi kwa kushinda michezo inayofuata.

"Nilikaa na wachezaji wetu nikawaambia wangeonyesha angalau asilimia 60 tu ya uwezo walioonyesha katika mechi dhidi ya Al Hilal iliyochezwa Mauritania, basi mechi ile na MC Alger tungeshinda, lakini ndiyo mpira, leo wa-

INAENDELEA UK. 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042